SportPesa
TZS. 1,042,431,860
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Mtoto** aliwa na mbwa, wanakijiji wazika kichwa

UKURASA 3

Nipashe
Jumatano Machi 16, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580886
www.ippmedia.com
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



XAVI: AUBAMEYANG NI ZAWADI

UKURASA 21

# Rais Samia kuteta na Polepole kirefu

• **Amwapisha** ubalozi, kupatiwa mafunzo maalumu... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akimwapisha Humphrey Polepole, kuwa Balozi wa Tanzania nchini Malawi, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**


## Shabiki alivyouawa vurugu za uwanjani

UKURASA 2

YALIYOMO

UKURASA WA 2
KITAMBULISHO CHA TAIFA KUPANDISHWA HADHI

UKURASA WA 8
TBL KUWANUFAISHA WANAWAKE MAMIA WANAOLIMA ZABIBU



KESI YA SABAYA

## Mshtakiwa adai wakili alimtaka aseme uongo

UKURASA 3

MICHEZO **MAYELE AMTULIZA MZUKA NABI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Rais Samia kuteta kirefu na Polepole

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amewaapisha viongozi mbalimbali aliowateua juzi, akisema kuwa kabla ya Balozi wa Malawi, Humphrey Polepole, kwenda nchini humo, atakutana na kuteta naye kwa kirefu.

Mkuu wa nchi huyo alitoa kauli hiyo jana baada ya uapisho wa Balozi Polepole na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Waziri Kindamba, uliofanyika Ikulu Chamwino mkoani Dodoma.

Alisema Balozi Polepole kabla ya kwenda Malawi, ataingizwa darasani kwanza katika Chuo cha Diplomasia.

"Tunaendelea na kazi kwa 'ku-swipe' watu kwenye maeneo mbalimbali. Leo (jana) tumeapisha watu wawili; Balozi na Mkuu wa Mkoa. Mheshimiwa Balozi ninajua baada ya hapa watakuweka darasani kwanza pale Chuo cha Diplomasia. Utakapotoka pale, kabla ya kwenda Malawi nitakutana nawe. Kwa hiyo, tutazungumza kwa urefu," alisema.

Akitoa maagizo kwa Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Rais Samia alimtaka kuupandisha mkoa huo kimapato na kuhimiza masuala ya lishe, ambayo katika hotuba yake ya kufunga mwaka 2021, aliweka wazi kwamba Tanzania haifanyi vizuri.

"Kaongeze jitihada, nenda mbele. Njombe ni mkoa wenye kila kitu, kama utatulia utaweza kupandisha kipato kwa kiasi kikubwa. Kuna mambo mengi ya kuangalia pamoja na kwamba Njombe ni mkoa unaozalisha chakula kwa wingi kuna tatizo la lishe, hapo kaangalie vizuri.

"Huko nyuma nilifanya mkataba na wakuu wa mikoa na wamefanya kazi nzuri. Ninafikiria tena kufanya mikataba na wakuu wa mikoa kusimamia masuala ya lishe. Kwa hiyo kaliangalie," aliagiza.

Kuhusu chanjo ya UVIKO-19, Rais Samia alihimiza wananchi waendelee kuhamasishwa kuchanja.

"Pia usisahau suala la chanjo nenda jitahidi kushirikiana na wenzako kahamasishe watu wachanje. Kama mlivyosikia tayari kuna Omicron imeanza huko Asia na wakianza huko hawapo mbali kufika kwetu, ninaomba mkasimamie," aliagiza.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema Watanzania wana imani na viongozi hao walioapishwa kupitia utendaji kazi wao.

"Tunatambua mkuu wa mkoa ni kiongozi wa shughuli za serikali. Mkoa wa Njombe ni mkoa uliojipambanua kwa shughuli nyingi za uchumi ikiwamo kilimo, lakini shughuli za ujasiriamali ambazo wana Njombe wanashughulika nazo wakazi wote. Njombe pia ni mkoa ambao kiusalama unafanya vizuri."

"Kama msimamizi mkuu wa shughuli za serikali Njombe, tunaamini utaungana na wananchi na utawaongoza kuchochea maendeleo na kuimarisha ulinzi na usalama na shughuli zote utakazokabidhiwa kwa miongozo iliyoko na ya mkuu wa nchi," alisema.

Kuhusu Balozi Polepole, Majaliwa alisema: "Balozi kama nilivyosema mwanzo, Mheshimiwa Rais amekuamini kuwakilisha nchi Malawi. Kwa heshima aliyokupa, Watanzania wana matumaini makubwa kwa sababu Malawi nchi jirani, ni nchi ambayo tumeishi muda mrefu tukiwa na uhusiano mzuri lakini Malawi ina fursa nyingi za kiuchumi.

"Ukiwa mwakilishi wa Tanzania nchini Malawi, utaimarisha hali ya ulinzi na usalama kwa sababu kwenye mipaka yetu lazima iendelee kuwa salama ili wananchi wetu waishi kwa amani na kufanya kazi zao kwa usalama," alisema.

Alimtaka Polepole kuhakikisha nchi hizo zinajenga uhusiano na kuimarisha uhusiano wa kiuchumi na kitamaduni.



Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Jenerali mstaafu Davis Mwamunyange (kushoto), akishuhudia mkazi wa Bagamoyo akifungulia maji kama ishara ya utekelezaji wa mradi wa kusambaza maji kutoka Makongo hadi Bagamoyo, mkoani Pwani jana. Mradi huo unategemea kunufaisha wakazi zaidi ya 450,000 kwenye maeneo ya Bagamoyo, Vikawe, Mbweni, Madale, Mivumoni, Wazo na Goba. Kulia ni Mjumbe wa Bodi ya mamlaka hiyo, Evarist Ndikilo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Polisi waua, kujeruhi mashabiki uwanjani

**Na Waandishi Wetu**

MTU mmoja ameuawa kwa kupigwa risasi na wengine wawili kujeruhiwa katika vurugu zilizotokea wakati wa mechi ya fainali ya mpira wa miguu ya Kombe la Kumbukumbu la Dk. Livingstone iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma, ikihusisha Mwandiga FC na Kipampa FC ya Ujiji.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, James Manyama, alisema jana kuwa kutokana na vurugu hizo, risasi ilimpiga Juma Ramadhani na kusababisha umauti.

Alisema kuwa askari wa jeshi hilo walilazimika kujihami baada ya kuzidiwa nguvu na mashabiki hao, akidai kuwa licha ya risasi kupigwa juu, hawakuacha vurugu ikiwamo mashambulizi dhidi ya askari.

Kamanda Manyama alidai kuwa katika vurugu hizo, Koplo Subira aliangushwa chini na kujeruhiwa kwa jiwe kichwani kisha kujihami kwa kupiga risasi za moto.

Hata hivyo, baadhi ya mashuhuda wa tukio, akiwamo Janson Rwekaza, walidai kuwa nguvu iliyotumika ilikuwa kubwa kwa kuwa tayari mashabiki walikuwa wameshatulia, lakini askari waliingia na kuanza kufyatua mabomu na kupiga risasi za moto.

**KAULI YA ACT**

Kutokana na tukio hilo, Chama cha ACT-Wazalendo kimelilaani na kumwomba Rais Samia Suluhu Hassan aangalie namna ya kufumua Jeshi la Polisi kiutendaji, kisheria na kiuwajibikaji ili litoke kwenye kile walichokiita jeshi la nguvu na kuwa linalotoa huduma.

Taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa Kisekta Wizara ya Mambo ya Ndani wa ACT-Wazalendo, Mbarala Maharagande, ilibainisha kuwa chama hicho kinapendekeza kiundwe chombo huru cha kuangazia mwenendo wa polisi.

"Chombo hicho kiwe na jukumu la kupokea malalamiko ya wananchi kuhusu matendo ya polisi na kuyafanyia kazi kwa sababu leo polisi ikikosea, hakuna sehemu ya kupeleka malalamiko," alisema.

Pia kimetaka uchunguzi huru ufanyike na kamati huru ya uchunguzi iundwe haraka ili kuchunguza tukio hilo na waliolifanya wasimamishwe kazi na wakamatwe wakati uchunguzi unafanyika.

ACT-Wazalendo pia kimependekeza kuundwe kamisheni ya maadili ya Jeshi la Polisi ili kusimamia weledi na maadili katika utendaji wao wa kila siku.

Chama hicho kimeitaka serikali na polisi wabebe jukumu la matibabu na fidia kwa majeruhi wawili wa risasi ambao ni Omary Amrani na Nasifu Moshi.

"Serikali na polisi inapaswa kutoa fidia kwa familia za marehemu Juma Bichuka kwa sababu alikuwa ana familia na ndiye alikuwa tegemeo katika familia yake kabla ya kuuawa na polisi," alisema Maharagande katika taarifa yake hiyo.

***Imeandaliwa na Pendo Thomas (KIGOMA) na Romana Mallya (DAR)***

## Kitambulisho cha Taifa kupandishwa hadhi

**Na Maulid Mmbaga**

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imesema ina lengo la kukipandisha hadhi Kitambulisho cha Taifa kwa kuingiza mifumo ya vitambulisho vingine vyote ikiwamo kadi ya benki, leseni ya udereva na pasi ya kusafiria vipatikane kwenye kitambulisho kimoja.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Umma kutoka NIDA, Geofrey Tengeneza, alisema kitambulisho hicho kitakuwa kinabeba vitambulisho vingine vyote hadi bima ya afya, jambo litakalowasaidia Watanzania kuondokana na adha ya kubeba vitambulisho vingi.

"Hiki ndicho kitambulisho pekee chenye uwezo huo, hakuna kingine chochote kwani hiki kina sili kadi ambayo inatunza taarifa, ina uwezo wa ku accommodate (kuchukua) vitambulisho vingine vyote kwa hiyo tutafika mahali tukiambiwa tuonyeshe leseni ya udereva unampa kitambulisho anaingiza namba anaona kila kitu.

"Miaka ya mbeleni tutafika mahali ambapo wenzetu tayari wameshafika kitakuwa kikitumika kwenye ATM, kama E-Wallet, unaweka fedha zako unatunza humo, huna haja ya kutembea na vingine, pia kitakuwa kinakuruhusu kuingia kwenye milango ya elektroniki hutakuwa na haja ya kuwa na vitu vingine, tutafika huko hivyo kitambulisho hiki kitakuwa na thamani kubwa," alisema Tengeneza.

Akizungumzia kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, alisema mamlaka hiyo imefanikiwa ununuzi wa mashine mbili kubwa ambazo zimesaidia kuongeza kasi ya uchakataji wa vitambulisho.

Alisema mwanzo kulikuwa na malalamiko ya ucheleweshaji wa Vitambulisho vya Taifa akibainisha kuwa tatizo hilo lilikuwa linasababishwa na kupungua uwezo wa uzalishaji katika mashine walizokuwa wakizitumia.

Alisema awali walikuwa na mashine tatu ambazo uwezo wake wa uzalishaji ni vitambulisho 500 kwa saa na baada ya muda uwezo wake ulishuka hadi kufikia 250 hali iliyosababisha kasi ya uzalishaji na uandikishaji watu wanaohitaji kadi hizo kutoenda sawa.

"Katika jitihada za kuhakikisha tunaongeza kasi ya uzalishaji tumefanikiwa kupata mashine zingine kubwa mbili ambazo katika hatua ya mwanzo kuanzia mwezi Januari mwaka huu tunazalisha vitambulisho 1,000 kwa mashine moja kwa saa, na kwa mwaka uliopita hadi kufikia Februari mwaka huu tulikuwa tumezalisha zaidi ya vitambulisho milioni 3.5," alisema Tengeneza.

Vile vile, alisema idadi hiyo awali walikuwa wanazalisha kwa muda wa miaka mitatu tofauti na sasa, pia alieleza kuwa hiyo imewasaidia kusambaza vitambulisho vingi wilayani ili kuwafikia Watanzania wengi na malalamiko kwa sasa yamepungua.

Kadhalika, wanatarajia kuongeza uwezo zaidi wa kuzalisha vitambulisho hivyo hadi kufikia 4,000 kwa saa kutokana na mashine hizo uwezo wake kuwa ni 4,500 kwa saa, ambazo kwa mashine mbili ni 9,000 sawa na vitambulisho 144,000 kwa siku.

HABARI KITAIFA

## Watanzania wote 300 waondolewa Ukraine

**Na Faustine Feliciane**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, amesema serikali imefanikiwa kuwaondoa Watanzania wote 300 waliokuwapo nchi Ukraine kutokana na machafuko yaliyotokana na kuvamiwa na Urusi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kuelezea mafanikio ya wizara hiyo katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, Balozi Mulamula alisema jukumu la serikali kupitia balozi mbalimbali za Tanzania ni kuhakikisha wanawalinda Watanzania wote nje ya nchi. Alisema mpaka jana hakuna Mtanzania aliyekwama Ukraine na baadhi ya Watanzania hao wamefika nchini na wengine wapo nchi za Poland na Ujerumani.

Alisema asilimia 80 ya Watanzania waliokuwapo Ukraine ni wanafunzi na wapo walioomba waendelee na masomo yao Tanzania na wengine wanatafuta nafasi ya kusoma nchi za jirani na Ukraine.

"Katika wanafunzi hawa wengi wao walikuwa wanasomea udaktari, sasa kuendelea na masomo yao vyuo vya hapa nchini kuna utaratibu wake, lakini tunafahamu wapo wengine katika nchi kama Ujerumani na wengine Poland wanaangalia uwezekano wa kuhamia katika vyuo vya nchi hizo kuendelea na masomo yao," alisema Balozi Mulamula.

Aliwataka Watanzania kujenga utaratibu wa kujiandikisha katika balozi za Tanzania wanapokuwa nje ya nchi ili kuwa na taarifa.

Alisema serikali itaendelea kusimamia usalama wa Watanzania popote waliko kwa maslahi yao na taifa.

Akizungumzia mafanikio ya wizara hiyo, Balozi Mulamula alisema katika kipindi cha mwaka mmoja viongozi wakuu wa kitaifa walifanya ziara nje ya nchi na viongozi wakuu kutoka nchi mbalimbali na mashirika ya kimataifa waliitembelea Tanzania.

"Rais Samia alifanya ziara za kitaifa, kikazi na kiserikali katika nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu, Ufaransa, Ubelgiji, Marekani, Rwanda, Malawi, Zambia, Burundi, Kenya na Uganda," alisema Balozi Mulamula.

Alisema katika ziara ya Rais Samia Ubelgiji Wizara yake iliratibu na kufanikisha uwekwaji saini wa mikataba sita yenye thamani ya Sh. trilioni 1.7 na upatikanaji wa Euro milioni 425 kutoka kamisheni ya Umoja wa Ulaya.

"Kwa pamoja mikataba na fedha hizo zitahusisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa awamu ya tano ya barabara za mabasi ya mwendo wa haraka, kuimarisha mifumo ya kidigitali, kuimarisha miji (Green Cities) pamoja na miradi mingine ya maendeleo katika sekta ya afya na kilimo," alisema Balozi Mulamula.

Alisema mafanikio mengine ni kusainiwa hati ya makubaliano 36 kati ya Serikali ya Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu, hati 12 zilisainiwa.

## Mtoto aliwa na mbwa, wakazi wazika kichwa

**Na Ibrahim Yassin,** KYELA

MTOTO mchanga anayedaiwa kutupwa na mwanamke asiyefahamika, ameliwa na mbwa na kubakizwa kichwa, kilichozikwa na wanakijiji wa Ikulu, Kata ya Ipinda wilayani Kyela mkoani Mbeya.

Akizungumza jana na Nipashe kijijini huko, mmoja wa mashuhuda wa tukio hilo, Miluna Mwaipopo, ambaye ni balozi wa eneo hilo, alisema walibaini hali hiyo juzi majira ya saa saba mchana baada ya kuona mbwa koko anatafuna nyama na alipofuatilie, aliona kimebaki kichwa cha mtoto mchanga.

Alisema kuwa baada ya kuona kichwa hicho, alipiga simu ofisi ya kijiji na viongozi walifika eneo hilo kujionea hali hiyo iliyowashangaza wengi kutokana na ukatili uliofanywa na mtu aliyetupa mtoto huyo.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho cha Ikulu, Samson Mwaijumba, alisema kuwa baada ya kupigiwa simu na balozi, alifika eneo hilo akiwa na Ofisa Mtendaji wa Kijiji na walisikitishwa kuona kichwa cha kichanga kikiwa na damu, huku sehemu nyingine ya mwili ikiwa imeliwa na mbwa.

Alisema bado hawajambaini mwanamke aliyefanya ukatili huo, lakini ufuatiliaji umeanza kwa kuitisha mkutano katika eneo hilo ili kuchunguza wanawake waliokuwa na ujauzito na maendeleo yao.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Ipinda, David Mlawa, alilaani kitendo cha kutupa watoto wachanga, akisisitiza kuwa mtoto huyo alikuwa na haki ya kimsingi ya kuishi.

"Suala hili limehuzunisha wengi na Mungu anakataza. Alifanya starehe zake halafu anafanya mauaji kwa mtoto asiye na hatia. Tunataka aliyefanya hivyo akamatwe, mkutano ufanyike katika eneo hili ili kumbaini," aliagiza.

Diwani wa kata hiyo, Elia Mwaipetania, aliunga mkono hatua zilizochukuliwa na uongozi wa kata na kijiji kumbaini aliyefanya unyama huo.

Alisema kuna dalili kuwa mwanamke huyo alitekeleza unyama huo muda mfupi baada ya kujifungua kwa kuwa eneo la tukio kumekutwa damu.

KESI YA SABAYA

# Mshtakiwa adai wakili alimtaka aseme uongo

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHAHIDI wa tano wa Utetezi, Watson Mwahomange (27), amedai alipofikishwa mahakamani na kusomewa maelezo ya awali, alikana kupeleka pampu kutengenezwa kwenye karakana ya mfanyabiashara Francis Mroso kwa kuwa alielekezwa kusema uongo na wakili wake, Fridolin Bwemelo.

Vilevile, amedai walikamatwa mkoani Dar es Salaam na Hemed Shaban, Ofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), akiwa na mshtakiwa wa kwanza katika kesi hiyo ya uhujumu uchumi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya.

"Ni kweli tulikamatwa na Hemed Shaban huko Dar es Salaam tukiwa watu sita ambao ni mimi, Sabaya, Silvester Nyegu, Enock Togolani, mke wa Sabaya na Saitabau na ofisa huyo wa TAKUKURU alikamata simu zaidi ya 10," alidai.

Shahidi huyo ambaye ni mshtakiwa wa tatu alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Dk. Patricia Kisinda, katika kesi hiyo ya uhujumu uchumi namba 27.

"Ni kweli kwamba Januari 20, 2021 nilipeleka pampu kwa Mroso kutengenezwa na nilitumwa na Sabaya na niliandika jina katika kitabu cha wageni," alidai.

Akihojiwa na Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, alidai kwamba Juni 6, 2021, alifikishwa mahakamani na kusomewa mashtaka ya kuongoza genge la uhalifu na utakatishaji wa fedha.

Alidai kwamba kabla ya kufikishwa mahakamani, alikuwa anafahamu Sabaya na Silvester Nyegu.

Shahidi huyo alidai mahakamani kwamba wakati akifishwa mahakamani Novemba 16, 2021, aliambiwa na wakili wake kukataa kila kitu isipokuwa kukubali kuwa alikamatwa na kufikishwa mahakamani.

Vilevile, alidai kwamba awali wakili alimweleza kwamba akikubali mashtaka hayo angelifungwa.

Pia alidai kwamba anamfahamu Sabaya na washtakiwa wengine kwa kuwa walikamatwa nao Dar es Salaam.

Shahidi huyo alidai kwamba Julai 16, 2021 Ofisa wa TAKUKURU, Ramadhani Juma, alikwenda magereza na alizungumza naye wakati kina Sabaya na wenzake wawili walikwenda mahakamani kwenye kesi nyingine iliyokuwa inawakabili.

Alidai kuwa aliposomewa maelezo ya awali, alikana kupeleka pampu na kukamatwa Dar es Salaam kwa kuwa yalikuwa ni maelekezo ya wakili wake.

Alidai kwamba alipofungwa pingu na kupelekwa katika karakana ya mfanyabiashara Francis Mroso, Januari 22, 2021, hakuona kama Ramadhani Juma alikuwa katika eneo hilo kwa kuwa hakwenda kuangalia watu.

"Siku hiyo nilikuwa nimefungwa pingu na walinipiga na baada ya hapo walinifungua pingu ndani ya gari ya Sabaya VX Masai, na wakanibebesha boksi la pampu kunipeleka katika ofisi ya Mroso," alidai.

Shahidi huyo alikana kuahidiwa kwamba atatolewa katika kesi hiyo na kupewa Sh. milioni 10 na Ramadhani Juma.

Alidai kwamba ni kweli Sabaya alikwenda kwa Mroso kama ilivyodaiwa na mashahidi wa mashtaka na kwamba mshtakiwa mwenzake huyo alikwenda kwa mfanyabiashara huyo akiwa na gari ya serikali lililokuwa linaendeshwa na dereva wa serikali aliyemtambua kwa jina moja la Kivuyo.

Pia alidai Sabaya ni mtu hatari sana na analitambua hilo hata kabla ya Januari 20, 2021 kwa kuwa alimpiga, akishirikiana na walinzi wake, kumweka mahabusu na kwa kipindi chote alikuwa akiishi kama mateka.

"Siwezi kusema afungwe kwa kuwa mahakama ndio itatoa uamuzi na siyo mimi," alidai.

Shahidi huyo alidai kuwa mwaka 2020 aliwahi kupigwa na kuvunjwa mguu na Sabaya.

CSDR Settlement & Custody

CSD & REGISTRY COMPANY LIMITED

TAARIFA KWA UMMA

KUSITISHA UTOAJI WA RISITI YA UWEKAJI

Tunapenda kuwafahamisha Mawakala wa Soko la Hisa la Dar es salaam (DSE), Benki zinazotunza dhamana za wawekezaji, Kampuni za uwekezaji, Taasisi za Fedha, Wawekezaji na Wananchi kwa ujumla kuwa, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) imepitisha Kanuni mpya za Soko la Hisa na Hifadhi ya Dhamana, (DSE – CSD Rules 2022). Hivyo kuanzia tarehe **1 Aprili 2022,** CSDR itasitisha utoaji wa Risiti ya Uwekezaji **(Depository Receipt)** maarufu kama Cheti cha Hisa kwa hisa zote zitakazonunuliwa kwenye Soko la Pili (yaani DSE).

Badala ya Risiti ya Uwekezaji (Depository Receipt), CSDR itatoa Taarifa ya Akaunti kama uthibitisho wa umiliki wa dhamana kwa mwekezaji. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 5(1) inayosema ***"Taarifa ya Akaunti inayotolewa na CSDR itakuwa ndiyo uthibitisho wa umiliki wa dhamana husika"***

CSDR itaendelea kutuma Taarifa ya Akaunti moja kwa moja kwa wanahisa kwa barua pepe kila mwisho wa mwezi. CSDR inatoa wito kwa Wanahisa wote kuwasiliana na Mawakala wa Soko la Hisa ili kuhuisha taarifa zao za mawasiliano ikiwemo anuani, namba ya simu na barua pepe ili kuwezesha utumaji wa Taarifa za Akaunti.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na:

Mkurugenzi Mkuu,
CSD & Registry Company Limited (CSDR),
Mtaa wa Ufukoni, Jengo la Kambarage, Ghorofa ya Pili,
S. L. P 70081,
DAR ES SALAAM
Simu: 0746 160516 / 0677 070414
Barua pepe: info@csdr.co.tz

216747402

# Mpango aonya viongozi uharibifu miradi ya maji

**Na Jaliwason Jasson,**
SIMANJIRO

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amewaonya viongozi wa umma na wananchi wanaoharibu kwa makusudi miradi na miundombinu ya maji inayojengwa kwa fedha nyingi na serikali kuwa wajiandae kuadhibiwa.

Dk. Mpango alitoa onyo hilo jana alipozindua mradi wa Maji wa Orkesmet ulioko Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara uliotekelezwa kwa Sh. bilioni 41.5.

"Niwaombe sana wananchi mtunze miundombinu ya maji na watakaokiuka watachukuliwa hatua kali. Viongozi wangu wa mkoa, simamieni hili na kupanda miti rafiki katika vyanzo vya maji. Ipo siku nitawashtukiza kuja kutembelea masoko na maeneo mbalimbali. Watakaobainika kuharibu, wawe viongozi, wawe wananchi wataadhibiwa," alisema.

Akiwa Orkesmet, Makamu wa Rais alimtaka Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, kuwa mkali katika kutunza mazingira.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso alisema wananchi wa Orkesumet walikuwa wanatembea kilomita 40 wakitumia punda kusaka maji.

Kutokana na kutambua mchango wa jitihada za wataalamu waliosimamia miradi aliyoiita kichefuchefu ya maji, Aweso amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Antony Sanga, kumpa zawadi ya Sh. milioni tano Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Babati (BAWASA), Iddy Msuya.

Msuya ndiye aliyesimamia utekelezaji na kuokoa Sh. bilioni 2.2 kwenye Mradi wa Maji wa Darakuta/Magugu.

Pia Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira (RUWASA), Wolta Kirita, aliangukiwa na neema hiyo ya kutuzwa Sh. milioni tano kwa kuokoa Sh. bilioni 1.5 za Mradi wa Maji Mayoka/Minjingu.

Awali, akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo wa Orkesmet, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Sanga, alisema mradi huo una uwezo wa kuzalisha lita milioni 6.720, wakati mahitaji yao ni lita milioni 1.5.

Sanga alisema maji hayo yanasukumwa na pampu kubwa tatu na kwamba mradi huo utawanufaisha zaidi ya wananchi 52,000.

Mbunge wa Simanjiro (CCM), Christopher Ole Sendeka, akizungumza katika hafla hiyo, alisema wazo la mradi huo wa maji liliasisiwa na aliyekuwa Waziri Mkuu wa zamani, Edward Sokoine.



Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, akicheza wimbo wa kabila la Wamasai, kabla ya kuweka jiwe la msingi la mradi wa maji wa Orkesumet, katika eneo la Loiborsoit wilayani Simanjiro, mkoani Manyara jana. Kulia kwake ni Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Charles Makongoro Nyerere. **PICHA: OMR**

# Mzunguko wa fedha waongeza ukwasi nchini

**Na Waandishi Wetu,**
ARUSHA

MZUNGUKO wa fedha katika uchumi umeongeza ukwasi kwa wananchi kwa wastani wa asilimia 9.3 kutokana na fedha zilizotolewa na serikali kwa kila halmashauri nchini, kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano ya UVIKO-19.

Jana, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akieleza mafanikio ya mwaka mmoja wa Rais, Samia Suluhu Hassan, alisema jambo hilo ukimuuliza mtu yeyote ambaye yuko eneo la mradi, atasema kwamba ameona na imeongezekaje.

"Wote tunajua habari ya trilioni 1.3. Nitolee mfano, ili kwenda vijijini kujenga shule shikizi na wakandarasi wanatokea humo humo kwenye vitongoji.

"Kujenga vituo vya afya kwenye kata zetu, Makandarasi wametoka humo humo, sio nje ya nchi. Wamejenga madarasa ambayo jumla yake ni 15,000 na wakandarasi wametoka kule kule vijijini.

"Hii fedha ilitoka IMF (Shirika la Fedha Duniani), nayo haiko hapa Tanzania, ikaja Tanzania ikaenda vijijini, maana yake hiyo fedha imeenda kwenye mzunguko wa fedha wa ndani ya nchi, kwa sababu hao waliofanya hiyo kazi, waliwalipa wale wanaosaidiana nao kufanya kazi pamoja na shughuli nyingine za kijamii ambazo wanazifanya."

Akieleza zaidi kuhusu ukwasi kuongezeka, Waziri Dk. Nchemba, alisema mfano mzuri ni sherehe za Krismasi na Mwaka Mpya, ambako maeneo mengi watu walilazimika kuomba kiti cha nyongeza, kwa sababu kulikuwa hakuna mahali pa kukaa.

"Wakandarasi wengi walishapoteza matumaini kwamba fedha zao wanaoidai serikali hazitalipwa. Madeni yao yamehakikiwa yote na yameshalipwa, ila kwa wale ambao bado uhakiki unaendelea."

**FEDHA ZA KIGENI**

Waziri Dk. Nchemba alisema fedha za kigeni zimeongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 6.4 Desemba 2021, ikilinganishwa na Dola za Marekani bilioni 6.0, Desemba 2020.

"Kwa hiyo hiyo na yenyewe imeongezeka, ambapo hiyo bilioni 6.6, kwa ulinganifu wa kiuchumi ni kiwango kinachoruhusu kuagiza bidhaa kwa miezi isiyopungua 6.6 kutoka nje ya nchi. Hicho ni kiwango cha juu kwa viwango vyetu vya Afrika ya Mashariki na vile vya SADC (Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika)," alisema.

"Tangu serikali ya awamu ya sita iingie madarakani, mapato yameongezeka kwa kiwango kikubwa sana, mtakumbuka Rais Samia, wakati anaapishwa alisema hataki fedha za mfukoni za kuendesha serikali, kwamba makusanyo yafanyike kwa weledi na kwa kuzingatia sheria.

"Mpaka Februari 2022, mapato ya ndani yameongezeka na kufikia trilioni 15.9 sawa na asilimia 93.5 ya makadirio ambayo yalikuwa yamewekwa kipindi hicho, ukilinganisha na trilioni 13.7 katika kipindi kama hicho na trilioni 11.6 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2020/2021."

**KUPAA GHARAMA ZA MAISHA**

Dk. Nchemba alisema, mfumuko huo hakujatokana na tatizo la kisera lililojitokeza na kusababisha gharama hizo kupanda, wala hakuna uamuzi wa kiutawala wa ndani ya nchi uliosababisha gharama za maisha zipande.

"Majanga ya dunia yakitokea, watu wote waungwana huwa hawanyoosheani vidole kwa sababu majanga yamekuja, wanamuomba Mungu awaepushie majanga na wanamuomba awape nguvu ya kukabiliana nayo.

"Kabla ya Machi 2019 wakati wa Covid-19, ngano kwa kilogramu 100 ilikuwa ni takribani Sh. 100,000, ikaingia vita ya Urusi na Ukraine; hiyo hiyo iliyokuwa around 100,000 kwenda chini, iko 140,000 na zaidi. Hapo ni kule kabla ya kuja na kusafirishwa imfikie mtu wa Kigoma."

"Sasa weka yule atakayebeba kwenye meli mpaka bandarini, weka na yule atakayebebaa kutoka bandarini mpaka kule kwa mlaji."

Kwa upande wa mbolea, Waziri Dk. Nchemba alisema: "Nenda kwenye mbolea, kwa mfano mbolea ya DAP ya mfuko wa kilogramu 50 ilikuwa Sh. 57,000 kabla ya Covid-19, sasa hivi ukiwa pale kwa mzalishaji, inauzwa kwa bei ya Sh. 110,000.

***Imeandikwa na Godfrey Mushi na Cynthia Mwilolezi**

# Ulinzi waimarishwa mpaka wa Msumbiji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Tax, amesema kwa sasa hali ni shwari katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji baada ya kuimarishwa ulinzi na usalama kutokana na tishio la ugaidi.

Dk. Tax alibainisha hayo jana jijini hapa alipoeleza mafanikio yaliyopatikana ndani ya mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema katika kipindi hicho, wizara hiyo kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), limeendelea kuimarisha ulinzi wa mipaka ya nchi na ipo shwari.

"Kumekuwapo na changamoto chache katika baadhi ya mipaka, hususan mpaka wa Kusini, hata hivyo changamoto hizo zimeshughulikiwa ipasavyo na hali ya amani na utulivu imeendelea kutamalaki.

"Tumekuwa na changamoto katika mpaka wetu wa Msumbiji, kikubwa kimekuwa ni ugaidi hasa upande zaidi wa wenzetu lakini kwa pamoja tumeshirikiana na kupitia makubaliano tuliyonayo kikanda tumeweza kushirikiana na kudhibiti,"alisema.

Waziri huyo alibainisha kuwa JWTZ inashirikiana na misheni ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika - SADC (SAMIM) katika kupambana na ugaidi Msumbiji.

Alisema serikali imeendelea kudumisha ushirikiano wa kimataifa na kitaifa katika sekta ya ulinzi katika kushiriki oparesheni mbalimbali za ulinzi wa amani kwenye nchi zenye migogoro.

Akizungumzia vijana wa JKT waliosimamishwa kwa utovu wa nidhamu na baadaye kusamehewa, waziri huyo aliweka bayana mambo yaliyolisukuma jeshi kuwasamehe vijana hao 854 ikiwamo kuwafuatilia kwa kina.

"Walifuatiliwa kwa kina sana na jeshi lilijiridhisha wanaweza kupewa nafasi kutokana na mienendo yao kuridhisha, pia sababu nyingine ni serikali kutambua mchango wao ambapo wakati wakijitolea walishiriki ujenzi wa miradi mbalimbali ya kimaendeleo," alisema.

Waziri huyo alisema migogoro ya ardhi 74 kati ya jeshi na wananchi imetatuliwa kwenye maeneo mbalimbali nchini huku Sh. bilioni 8.015 zikitumika kulipa fidia wananchi.

"Uthamini na uhakiki umekamilika katika maeneo mengine ya Ras Nondwa (Kigoma), Nyagungulu (Mwanza), Nyamisangura (Tarime), Usule (Tabora) na Duluti (Arusha) wenye thamani ya Sh. bilioni 10.44. Maeneo 50 yamekwishafanyiwa upimaji na uthamini na ambayo uhuishaji wa mipaka na uhakiki unaendelea," alisema.

Aliongeza kuwa wizara na taasisi zake imetoa ajira zaidi ya 9,341 kupitia miradi mbalimbali ya kudumu na ya muda mfupi.

## Waomba elimu ya malezi watoto njiti

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WADAU wanaoshughulika na masuala ya watoto njiti wameiomba serikali kuona umuhimu wa kutoa elimu inayohusu masuala ya watoto hao kuingizwa kwenye mitaala kuanzia darasa la tano katika masomo ya Sayansi na Baiolojia.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Doris Mollel Foundation, Doris Mollel, alitoa ushauri huo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa alipokutana na wadau wa elimu wakiwamo wakuza mitaala kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania (TET).

Alisema kwa kufanya hivyo kutasaidia kujenga uelewa mpana wa jamii na kupunguza ongezeko la watoto hao pamoja na kufahamu namna bora ya malezi yao ili waondokane na changamoto mbalimbali zinazowakabili ambazo nyingine zimewasababishia vifo au kuwa walemavu.

Alisema ipo haja pia ya kurekebishwa kwa sheria ya uzazi kwa kuongezwa zaidi muda wa miezi mitatu iliyoko sasa kwa mama na siku tatu za baba ili kusaidia zaidi malezi ya karibu kwa watoto hao ambao hutumia muda mwingi kukaa hospitali kwa huduma.

Alisema taasisi hiyo imekuwa ikisaidia serikali kupunguza vifo vya watoto wachanga nchini hususani vinavyotokana na kuzaliwa kabla ya wakati na imekuwa ikifanya hivyo kupitia utoaji wa elimu kwa jamii, kuchangia vifaa tiba na kushauri serikali namna bora za kisera za kusaidia wazazi wanaopata changamoto ya kupata watoto kabla ya wakati.

"Tulifanya utafiti kwa shule kumi 10 za Tanzania bara tukabaini wanafunzi hawana ufahamu wowote kuhusu suala la watoto njiti, tumeanza kuwaelimisha wafahamu mapema elimu hii kwasababu wanachofundishwa sasa ni masuala ya mimba na masuala ya afya ya uzazi tu," alisema Mollel.

Pia alisema wanashirikiana na TET kujadili umuhimu wa kuweka elimu ya mtoto njiti kwenye mtaala wa masomo na kusisitiza mtoto njiti anahitaji uangalizi maalumu na wa karibu kuanzia anapozaliwa mpaka ukubwa na kuepuka changamoto mbalimbali za kiafya.

Daktari wa masuala ya watoto, Robert Moshiro kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, alisema sababu za kuzaliwa watoto njiti na namna ya kukabiliana na hali hiyo kuwa ni pamoja na magonjwa sugu kama kisukari, shinikizo la damu (kifafa cha mimba), lishe duni, upungufu wa damu, maambukizi njia ya haja ndogo (UTI), kifua kikuu TB, Ukimwi, malaria, utoaji mimba wa mara kwa mara na maambukizi ya ukeni.

Alisema mtoto njiti anahitaji matunzo ya kipekee kama huduma muhimu za awali baada ya kuzaliwa, kutunza kiwango cha joto mwilini, kwa kumpatia hewa ya Oxygen au zaidi njia ya kienyeji inayotumika sasa ya kangaroo ya mama kugusana ngozi na mtoto kwa kumuweka kifuani, kutumia kiwango cha maji mwilini na lishe hasa maziwa ya mama.

Dk. Moshiro alisema nchini Tanzania kati ya watoto milioni 2.6 wanaozaliwa kila mwaka, kati yake 250,000 huzaliwa njiti sawa na mtoto mmoja kati ya kumi wanaozaliwa.

Kati ya watoto wote njiti wanaozaliwa, 9,500 hufariki kila mwaka sawa na mtoto mmoja kwa saa.

# Watumiaji huduma fedha kimtandao wafikia mil.35

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imesema, watumiaji wa huduma za fedha kwa njia ya simu, wameongezeka na kufikia milioni 35.2.

Aidha, imeondoa gharama za majaribio kwa wanafunzi katika ubunifu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kupata matokeo chanya yatakayosaidia ukuaji wa uchumi nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabir Bakari, aliyaeleza hayo jana mkoani Dar es Salaam, wakati akifungua Maadhimisho ya Siku ya Haki za Watumiaji Duniani.

"Idadi ya wanaotumia simu za mkononi kufanya miamala ya fedha imeongezeka na hadi Februari mwaka huu, watumiaji walikuwa milioni 35.2 kulinganisha na miaka ya nyuma," alisema Dk. Bakari.

Kuhusu kuondoa gharama za majaribio alisema tayari ameshafanya mazungumzo na kampuni zote za simu kuwa wanafunzi watakaofanya bunifu hizo kupitia mtandao wasitozwe gharama yoyote.

"Nimeshazungumza na kampuni za simu kuwa wanafunzi wasichajiwe gharama yoyote, lengo ni kupata matokeo chanya katika uchumi wa kidigitali," alisema Dk. Bakari.

Alisema, sekta ya mawasiliano imekuwa ikitumika kuhudumia uchumi wa fedha na sasa hivi unaweza kutumia kama benki inayotembea ikiwamo kulipa kodi na tozo za serikali.

"Ukuaji huu umesaidia kupeleka uchumi mbele, ongezeko hilo linatoa picha kuwa watumiaji wa mtandao wa huduma za fedha wanakuwa siku hadi siku," alisema.

Alisema TCRA, itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kulinda haki za walaji pamoja na kuandaa mazingira ili pawe na utumiaji wenye manufaa na uweze kukua kwa haraka.

Naye Mkurugenzi wa Leseni na Ufuatiliaji TCRA, John Daffa, alisema walianza maadhimisho hayo kwa kuwakutanisha wadau mbalimbali wa sekta ya mawasiliano kwa ajili ya kutatua changamoto mbalimbali katika sekta hiyo.

Alisema maadhimisho hayo yamefanyika kwa mara ya kwanza na utaratibu huo utakuwa endelevu.

Maadhimisho hayo yameambatana na uzinduzi wa klabu mbalimbali za kidigitali lengo likiwa ni kuwawezesha wanafunzi kufahamu matumizi sahihi ya mtandao.



Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Mkonge nchini, Saad Kambona (kulia), akizungumza na wakulima wa zao hilo, mbele ya Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde (wa pili kulia), alipotembelea shamba la mkonge la Magunga, Wilayani Korogwe, mkoani Tanga jana. Kushoto ni Mwenyekiti wa Magunga Amcos, Shadrack Lugendo na (wa pili kushoto) ni Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Basila Mwanukuzi. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# FCC yaagizwa kuzuia wizi fedha mtandaoni

**Na Richard Makore,** MWANZA

SERIKALI imeagiza Tume ya Ushindani Nchini (FCC) kwa kushirikiana na vyombo vingine kufanya utafiti ili kupata mifumo bora ya kuzuia wizi wa fedha kwa njia ya mtandao hapa nchini.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini hapa na Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, katika maadhimisho ya kilele cha Siku ya Kumlinda Mtumiaji Duniani.

Dk. Kijaji alisema bado jamii inasumbuliwa na ulaghai na wizi wa kimtandao na kuitaka FCC kwa kushirikiana na vyombo vingine wafanye utafiti wa kina ili kukabiliana na janga hilo la kitaifa na kidunia. Aliongeza kuwa ili jamii iwe salama katika utumiaji wa huduma za fedha kwa njia ya kiditali, inapaswa kufuata mifumo imara iliyowekwa na serikali.

Alisema masuala ya utakatishaji fedha pamoja na ugaidi duniani yanafanyika kwa kutumia teknolojia ya kisasa na vyombo vilivyopewa dhamana kusimamia sheria vinatakiwa kuliona hilo na kuliwekea misingi imara ya kupambana nalo.

"Utakatishaji wa fedha unaharibu kabisa uchumi wa nchi na suala hili ni lazima kama nchi tupambane nalo ili kulimaliza katika jamii yetu," alisema Dk. Kijaji.

Dk. Kijaji aliwataka watoa huduma za fedha wote kuweka mifumo itakayolinda watumiaji ambao ni wateja wao.

Alipongeza Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa kuendelea kuwa na mifumo imara ya kulinda watoa huduma za fedha wa ndani na nje ya nchi.

Alisema ifikapo mwaka 2024 watu bilioni 3.6 duniani kati ya bilioni saba watakuwa wanatumia huduma za fedha kwa njia ya kidigitali.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya FCC, Dk. Agrey Mlimuka, akizungumza katika siku ya kumlinda mtumiaji, alisema wataendelea kusimamia haki katika ushindani wa kibiashara.

Alisema ili wafanyabiashara nchini waweze kushindana ni lazima FCC isimamie kanuni na sheria zilizowekwa.

Wadau mbalimbali wakiwamo wafanyabiashara, wanasheria na wawakilishi wa taasisi za umma walishiriki katika sherehe hiyo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni mwanzo mzuri marekebisho Sekta ya Habari, Mawasiliano

**JUZI,** Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alizungumzia mafanikio ya mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita, tangu ilipoingia madarakani Machi 18, mwaka jana.

Mojawapo ya mafanikio aliyotaja ni pamoja na serikali kufanya marekebisho ya Kanuni za Utangazaji kwa njia ya Kidijitali za mwaka 2018, ili matangazo ya televisheni yawafikie wananchi wengi na kuvutia uwekezaji kwa vyombo vya utangazaji.

Kwenye maelezo yake, Waziri Nape alisema marekebisho hayo ni kuruhusu watoa huduma wanaotoa maudhui ya bila malipo kwa wananchi kubebwa katika ving'amuzi vya kulipia kama vile DSTV na Zuku.

Alisema huko nyuma televisheni hizo zilikuwa zikibebwa na watoa huduma wenye miundombinu ya ardhini pekee, hivyo kusababisha kutokuonekana kwenye ving'amuzi vya setilaiti na kwamba mabadiliko hayo yameongeza wigo wa chaneli zaidi ya 14 kuonekana kwenye ving'amuzi vya setilaiti

Pia, alisema serikali imeondoa hitaji la leseni ya 'simulcasting'. Hii ni kwa watoa huduma wa maudhui wanaotoa maudhui kwa njia ya redio ama televisheni wanapotaka kwa wakati huohuo kutoa matangazo hayo kwa njia ya mtandao hawatahitaji leseni nyingine.

Alitangaza serikali kufanya marekebisho ya kuondoa leseni kwa watoa maudhui mbalimbali ikiwamo mapishi, michezo, usanii kama vile muziki.

Kadhalika, alitangaza kufanyika kwa marekebisho ya kanuni za maudhui ya mtandaoni za mwaka 2020 lengo kuu likiwa ni kukuza ajira na vipaji kwa vijana wa kitanzania.

Kuondolewa kwa zuio la wageni kutembelea studio zinazorusha matangazo na kutoa maudhui pasipo kuambatana na ofisa wa serikali.

Uamuzi wa kufanya maboresho hayo ni hatua nzuri katika kuiinua kiuchumi sekta ya habari na mawasiliano kusonga mbele.

Tunampongeza Waziri Nape na Serikali ya Awamu ya Sita kwa hatua hiyo nzuri ambayo inajenga na kukuza sekta ya habari kwa sababu kwa kufanya hivyo kutaongeza ajira kwa vijana wengi wa kitanzania, pamoja na kuongeza matangazo kwa vyombo vya habari hususani ya televisheni.

Si hilo tu, uamuzi wa kurudisha chaneli za nyumbani katika ving'amuzi vyote kumeibua shangwe kwa Watanzania wengi ambao walikuwa wakitaabika kupata taarifa za nyumbani, hali iliyokuwa ikiwalazimu kulipia gharama fulani ili kupata huduma hiyo.

Kadhalika, serikali imefanya marekebisho ya kanuni za maudhui ya mtandaoni za mwaka 2020 ikiwamo kupunguzwa kwa ada ya maombi ya leseni kutoka Sh. 1000,000 hadi 500,000 na ada ya mwaka kutoka Shilingi milioni moja hadi Sh. 500, 000.


Kwa mujibu wa Waziri Nape marekebisho ya kanuni hizo ni kukuza fursa, ajira na vipaji kwa vijana wa kitanzania.

Ni kweli kwa marekebisho ya kanuni na sheria hizo kutaongeza ajira kwa Watanzania wengi kwani awali kulikuwa na vizingiti vya kisheria na fedha za kuanzisha ama kurusha maudhui kwenye mtandao au moja kwa moja.

Serikali kupitia Waziri Nape imewahakikishia Watanzania mambo mengi mazuri yanayokuja na kufanyiwa marekebisho ikiwamo kuwapo katika hatua ya mwisho za utungaji wa sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi kwa lengo la kusaidia na kufanikisha uchumi wa kidijitali na kwamba mapendekezo ya sheria hiyo yapo katika ngazi mbalimbali kwa ajili ya ridhaa.

Tunaamini huu ni mwanzo wa mambo mazuri mengi yanayotarajiwa kuja katika sekta ya habari, mawasiliano na teknolojia ya habari, kwa sababu wahenga wanasema dalili ya mvua ni mawingu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mwaka mmoja wa Rais Samia Ikulu akiwa makini kuwainua wanawake

Na Sabato Kasika

**ILIKUWA** siku, wiki, mwezi, sasa hatimaye umetimia mwaka tangu Rais Samia Suluhu Hassan ale kiapo cha kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuchukua nafasi iliyoachwa na mtangulizi wake, Dk. John Magufuli.

Katika kipindi cha mwaka mmoja, yapo mengi ambayo rais ameyafanya ikiwamo kuongeza wanawake katika baraza la mawaziri, kuwateua kuwa wakuu wa mikoa wilaya na wengine kwenye nafasi mbalimbali za uongozi.

Ninaamini kwamba, unapotimia mwaka mmoja wa uongozi wake, wanawake wanalo la kujivunia kwa jinsi ambavyo amefanya mageuzi kwa kuongeza idadi yao katika nafasi mbalimbali za uongozi na kukata kiu yao ya muda mrefu.

Usawa wa kijinsia ni miongoni mwa mambo makubwa ambayo wanawake wamekuwa wakiyalilia kwa muda mrefu kwa lengo la kutaka kuwe na uwiano kati yao na wanaume kwenye suala la uongozi.

Wanapoelekea kwenye mwaka mmoja wa Rais madarakani, ni vyema kuwambusha wale ambao wamefanikiwa kuteuliwa, waendelee kuonyesha umahiri katika uongozi ili kumfanya Rais aendelee kuwaamini.

Kimsingi, Rais amekuwa akijitahidi kuhakikisha anamwinua mwanamke kwa kuwateua wengi katika nafasi mbalimbali za uongozi kuanzia ngazi ya chini ili kuondoa dhana kwamba mwanamke hawezi kuongoza.

Hatua hiyo inaonyesha ni jinsi gani amedhamiria kumwinua mwanamke ili asiendelee kuwa mnyonge bali afanye kazi kama mwanaume, kutokana na ukweli kwamba, uongozi si mzigo bali ni akili na uwezo wa kuongoza.

> **Mwanamke ana majukumu makubwa nyumbani kuanzia kwenye kulisha familia na mengine mengi, kama anaweza hayo, atashindwaje kuongoza, hata kutokana na ukweli kwamba uongozi unaanzia nyumbani?**

Kwa mantiki hiyo, ni vyema wanawake ambao tayari wamepata nafasi za uongozi, watekeleze majukumu yao kikamilifu ili kujijengea sifa za kuwawezesha kuendelea kuteuliwa wengi zaidi.

Ukweli ni kwamba uongozi si kwa ajili ya kundi fulani au jinsia fulani bali watu wote wanaweza kuongoza awe mwanaume au mwanamke ili mradi awe na sifa zinazotakiwa ikiwamo elimu, weledi na uwezo wa kuongoza.

Vilevile si vibaya watunga sera na walioko katika ngazi za maamuzi kuhakikisha wanaondoa vikwazo ambavyo vimekuwa vikimfanya mwanamke kubaki nyuma ili kumsaidia Rais kutimiza lengo la usawa wa kijinsia.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba, suala la usawa wa kijinsia haliepukiki, kwa maana hiyo kila mbinu ambazo zinalenga kukwamisha juhudi za wanawake kufikia 50 kwa 50 ni vyema zikashindwa.

Mwanamke ana majukumu makubwa nyumbani kuanzia kwenye kulisha familia na mengine mengi, kama anaweza hayo, atashindwaje kuongoza, hata kutokana na ukweli kwamba uongozi unaanzia nyumbani?

Kwa kuwa Rais ameshapanua wigo kwa kuwapa wizara baadhi ya wanawake na wakaonyesha uwezo mkubwa katika kuongoza, ingependeza kama watazidi kupewa ushirikiano ili waendelee kutimiza majukumu yao kikamilifu.

Kama ambavyo wanawake wenyewe wamekuwa wakisema kuwa uongozi si misuli bali ni akili na uwezo wa kuongoza, kaulimbiu hiyo ingetumiwa na jinsi zote ili kuendelea kuhamasisha usawa wa kijinsia katika jamii.

Iwapo yale yote ambayo yamekuwa yakilalamikiwa na wanawake yataondolewa, dhana nzima ya Rais ya kutaka kumnyanyua mwanamke kuanzia msomi na asiye msomi, nadhani itakuwa imetimia.

Nirudie, watunga sera na walio katika ngazi za maamuzi, waangalie kila njia ya kuondoa vikwazo ambavyo vinaweza kujitokeza au kumbagua mwanawake katika uongozi, kwa ajili ya kuharakisha nchi kuwa na maendeleo endelevu.

# Serikali kushirikisha wadau kero ya maji

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imesema itashirikiana na sekta binafsi kuhakikisha miradi ya maji inakamilika ndani ya muda uliopangwa ili kuondoa changamoto ya upatikanaji wa huduma hiyo nchini.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, wakati akifungua mkutano wa wadau kutoka sekta mbalimbali ulioandaliwa na Shirika la WaterAid.

Alisema malengo ya wizara ni kuongeza kasi katika utekelezaji wa miradi aliyoibainisha ikiwamo kushirikiana na sekta binafsi kwa lengo la kukamilika ndani ya muda uliopangwa.

"Katika lengo hili wadau kama WaterAid wana mchango mkubwa katika kuhakikisha adhma ya wizara inafanikiwa na tupo pamoja nao," alisema.

Alisema wizara inajielekeza kwenye miradi mikubwa yenye vyanzo vya maji vya uhakika na itakayohudumia idadi kubwa ya wananchi.

"Kuongeza nguvu katika utunzaji wa vyanzo vya maji na juhudi kubwa katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kuongeza msukumo katika utekelezaji wa miradi ya majitaka na usafi wa mazingira mijini na vijijini," alisema.

Mahundi alisema hali ya upatikanaji wa maji kwa sasa imefikia asilimia 72.3 kwa vijijini na asilimia 86 kwa mijini.

Alisema kwa takwimu hizo bado wadau wana kazi kubwa ya kufanya katika kufikia malengo ya milenia hususani lengo namba sita la kuhakikisha kuwa majisafi na salama yanapatikana kwa watu wote ifikapo mwaka 2030.

Mahundi alitoa wito kwa wadau wote kuendelea kushirikiana ili kufikia lengo hilo na Watanzania kupata majisafi na salama na kuondokana na tatizo la kukosekana kwa huduma hiyo katika baadhi ya maeneo.

Aidha, alisema Shirika la WaterAid limekuwa likishirikiana na serikali katika kuongeza upatikanji wa huduma za maji, usafi wa mazingira na usafi binafsi (WASH).

"Serikali inatambua mchango mkubwa wa shirika hili na asasi zingine za kiraia ambazo tumekuwa tukishirikiana nazo katika sekta ya maji. Kuna msemo ukitaka kwenda haraka nenda peke yako lakini ukitaka kwenda mbali nenda na wenzako serikali inataka kwenda mbali hivyo imechagua kwenda na wenzetu kama WaterAid ili tuweze kufikia adhma yetu," alisema Mahundi.

Alisema mkutano huo muhimu una adhma ya kushirikisha kazi zinazofanywa na WaterAid nchini, kubadilishana mawazo, uzoefu na kushirikishana ujuzi na wadau mbalimbali waliopo nchini.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkaazi wa Shirika la WaterAid, Anna Mzinga, alisema wataendelea kutoa ushirikiano kwa serikali na wananchi ikiwamo makundi maalumu ili kupata huduma stahiki zenye tija endelevu za huduma za majisafi na mazingira.

"Shirika lina maono ya kuhakikisha watu wote wanapata huduma ya maji safi ya uhakika, vyoo bora na usafi binafsi wenye viwango na uhifadhi wa mazingira hususani katika vyanzo vya maji," alisema.

Mzinga alisema hadi sasa wamefanikiwa kuwafikia wananchi zaidi ya milioni nane wanaoishi maeneo ya mjini, pembezoni mwa miji na vijijini.

# Muhimbili yapongezwa kwa matumizi fedha za UVIKO-19

**Na Romana Mallya**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imepongezwa kwa utekelezaji wa fedha za UVIKO-19 ambapo hadi sasa imetia saini mikataba 57 na wazabuni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba.

Pongezi hizo zilitolewa juzi na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi, alipotembelea hospitali huko kuona utekelezaji wa fedha za UVIKO-19 Sh. bilioni 25.5 ilizopokea kwa ajili ya miradi na kupewa jukumu la kununua vifaa vya Hospitali za Rufani za Mikoa ya Amana, Temeke, Mwananyamala na Tumbi.

Baada ya kusomewa taarifa ya fedha, Prof. Makubi alisema Muhimbili imeonyesha dalili za moja kwa moja kwamba utekelezaji wa miradi utakamilika ndani ya muda husika ambao ni Aprili mwaka huu.

"Kasi ya utekelezaji wa miradi inaridhisha, nina matumaini makubwa kuwa miradi hii itakamilika ndani ya muda tuliojiwekea hata kama muda utazidi, nina imani hautakuwa zaidi ya wiki ya kwanza ya mwezi Mei," alisema.

Awali, akisoma taarifa za fedha hizo, Mkurugenzi Mtendaji wa Muhimbili, Prof. Lawrence Museru, alisema kati yake, Muhimbili ilipangiwa Sh. bilioni 11.87 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba zikiwamo MRI, CT-Scan, Angio suite, vifaa vya ICU, ujenzi na ukarabati wa idara ya magonjwa ya dharura na kitengo cha dharura kwa wajawazito.

Alisema hadi sasa wametia saini mikataba 16 na wazabuni yenye thamani ya Sh. bilioni 11.87.

Prof. Museru alisema kwa upande wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Temeke ilipangiwa Sh. bilioni 4.071 kwa ajili ununuzi wa CT-Scan, Digital X-Ray, Portable Ultrasound, vifaa vya ICU, radiolojia, vifaa vya idara ya magonjwa ya dharura na hadi sasa imetia saini mikataba 11 na wazabuni ya Sh. bilioni 3.5.

"Hospitali ya Rufani Mkoa wa Amana ilipangiwa Sh. bilioni 4,065 kwa ajili ununuzi wa CT-Scan, Digital X-Ray, Portable Ultrasound, vifaa vya ICU, radiolojia, vifaa vya idara ya magonjwa ya dharura na hadi sasa imetia saini mikataba tisa na wazabuni yenye Sh. bilioni 3.5," alisema.

Alisema Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mwananyamala ilipangiwa Sh. bilioni 1.8 kwa ajili ununuzi wa Digital X-Ray, Portable Ultrasound, vifaa vya ICU, radiolojia, vifaa vya idara ya magonjwa ya dharura na hadi sasa imesaini mikataba 10 na wazabuni ya Sh. Bilioni 1.7.

"Hospitali ya Rufani Mkoa wa Tumbi ilipangiwa Sh. bilioni 3.6 kwa ajili ununuzi wa CT-Scan, Digital X-Ray, Portable Ultrasound, vifaa vya ICU, radiolojia, vifaa vya idara ya magonjwa ya dharura hadi sasa Tumbi imetia saini mikataba 11 na wazabuni ya Sh.bilioni 3.5," alisema.




Mkazi wa Wilaya ya Tunduru, mkoani Ruvuma, Omary Mashaka Hassan (katikati), akifurahia na majirani zake, baada ya kukabidhiwa fedha zake Sh. Milioni 10, alizoshinda kwenye mchezo wa kubashiri wa Biko, wilayani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wataka muswada wa kufumua Sheria ya Ndoa

**Na Getrude Mbago**

TAPO la Wanawake na Wasichana Tanzania limeliomba Bunge litekeleze jukumu lake la kikatiba kwa kuitaka serikali iwasilishe bungeni muswada kwa ajili ya marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971.

Sheria hiyo inaruhusu mtoto chini ya miaka 18 kuolewa kwa ridhaa ya mzazi.

Wakizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wadau hao walisema licha ya serikali kupewa mwaka mmoja na mahakama kuibadilisha sheria hiyo, mpaka sasa bado hajatekeleza amri hiyo.

Mwanzoni mwa mwaka 2016, Rebeca Gyumi, Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali Msichana Initiative, alifungua kesi kupinga vifungu vya 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa vinavyoruhusu mtoto wa kike kuolewa akiwa na miaka 14 kwa kibali cha mahakama na miaka 15 kwa ridhaa ya wazazi, mtawalia.

Julai 8, 2016, Mahakama Kuu ilitoa hukumu, ikikubali kwamba vifungu hivyo vya Sheria ya Ndoa vinapingana na Katiba ya nchi kwa kuweka umri tofauti wa kuoa na kuolewa kati ya mtoto wa kike na wa kiume.

Gyumi alisema katika hukumu ya mahakama, iliitaka serikali kupitia kwa Mwanasheria Mkuu kujipanga ili kuvirekebisha vipengele hivyo tata vya sheria ndani ya mwaka mmoja.

"Lakini ni miaka mingi sasa imeshapita tangu amri hiyo itoke na hakuna jitihada zozote zilizofanyika katika kutekeleza uamuzi huo," alisema.

Dk. Dinah Mmbaga, mmoja wa wadau hao, alisema ni muda mwafaka sasa kwa wabunge kuchukua hatua na kuhakikisha serikali inaleta muswada huo wa marekebisho bungeni.

Alisema ndoa za utotoni zina madhara makubwa kwa wasichana kwa kuwa wengi hushindwa kutimiza ndoto zao na hivyo kuishia kupata maumivu ya unyanyasaji.

Tapo hilo linaundwa na mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali yanayopigania haki na ustawi wa wanawake na watoto wa kike nchini.

# TBL kuwanufaisha wakulima wanawake

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI ya Tanzania Distilleries Limited (TDL) inayojishughulisha na utengenezaji na uzalishaji wa mvinyo, kupitia miradi ya kampuni mama ya bia Tanzania (TBL), inatarajia kuingia kwenye kilimo shirikishi na wakulima 300 wa zabibu mkoani Dodoma mwaka huu.

Imebainisha kuwa kati ya asilimia 30 na 40 ya wakulima watakaoshirikishwa, watakuwa wanawake na itanunua tani 1,500 za zabibu kutoka kwa wakulima hao.

Mwanzoni mwa mradi huo ulioanzishwa mwaka jana, TDL ambaye ni mteja mkubwa wa zabibu na vilevile mzalishaji mkubwa wa mvinyo nchini, ilitumia jumla ya Sh. milioni 350 kwa ajili ya kununua tani 233 za zabibu kutoka kwa wakulima wanaoshirikiana kimkataba, TDL ikinunua zabibu hizo kwa Sh. 1,500 kwa kilo.

"TDL imekuwa mwanzilishi wa maendeleo ya sekta ya uzalishaji wa mvinyo nchini, na vilevile kujizatiti katika kuwawezesha wakulima wa zabibu nchini.

"Kwa sasa TDL ina uhusiano wa kibiashara na zaidi ya wakulima 700 wa zabibu ambazo zinatumika kutengeneza aina mbalimbali za mvinyo.

"Kupitia programu hii, TBL inalenga kukuza kilimo cha zabibu nchini huku ikilenga kuwezesha wanawake kiuchumi," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa TBL, Jose Moran alipozungumza na Nipashe jana.

Mmoja wa wakulima wanawake wa zabibu mkoani Dodoma aliyenufaika na programu hii ya uwezeshaji wanawake kwenye kilimo cha zabibu, Irene Madeje-Mlola, alisema: "Kwenye kilimo, taarifa ni muhimu sana, huwa tunatembelewa mara kwa mara na wataalamu kutoka TDL kutusaidia na mazao yetu, kutushauri kuhusu mambo mbalimbali ikiwamo matumizi ya mbolea bora, dawa za kuua wadudu shambani na vilevile kutoa msaada wakati wa mavuno."

Mkulima huyo aliongeza kuwa kwa kushirikiana na TDL, sasa wameweza kufanya majaribio mbalimbali kwenye shamba lao kujaribu njia mbalimbali za kuongeza uzalishaji pamoja na namna ya kudhibiti sehemu za udongo zilizoathirika.

Katika shughuli zake za uzalishaji, kampuni mama AB InBev inategemea mazao ya kilimo yenye ubora wa hali ya juu kutoka kwa jamii zinazostawi na mfumo mzuri wa ikolojia.

Kwa kupitia mfumo wa kujikita kushirikiana na wakulima katika mpango wake wa kuwezesha kilimo endelevu, AB InBev kupitia wakulima waliobobea katika masuala ya uchumi na watafiti, imelenga kufikia asilimia 100 ya wakulima wa moja kwa moja wenye uwezo na waliowezeshwa kiuchumi kufikia mwaka 2025, ambao kwa Tanzania ni ukomo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Juni 1999-2025.




Ofisa Mkuu wa Tigo Pesa, Angelica Pesha, akitambulisha promosheni mpya ya wiki iitwayo "Pesa Mwaa Mwii na Tigo pesa", jijini Dar es Salaam jana, ambayo itawawezesha wateja wa Tigo Pesa kuondoka na zawadi za fedha taslimu hadi Sh. milioni 325. Kushoto ni Meneja wa Wateja Maalumu wa Tigo Pesa, Mary Rutta. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Tani 18 za zebaki zatumika migodini

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI imesema wachimbaji wadogo wa dhahabu hutumia tani 18.5 za zebaki kila mwaka bila kuzingatia tahadhari, hivyo kuwa hatarini kuathiri afya za wananchi, mazingira na ustawi wa maendeleo endelevu ya nchi.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Edward Nyamanga, alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipofungua warsha ya uhamasishaji wa utekelezaji wa mpango kazi kitaifa wa kupunguza matumizi ya zebaki kwenye uchimbaji mdogo wa dhahabu (2020-25).

Alisema licha ya faida kubwa inayopatikana kutokana na sekta hiyo, shughuli za wachimbaji wadogo zimeibua matatizo mengi kwa afya ya binadamu na mazingira, ukiwamo umwagaji maji yenye sumu kwenye mazingira.

Nyamanga alisema mazingira yanakabiliwa na uchafuzi wa hewa unaotokana na uchomaji holela wa dhahabu, ukataji wa miti mikubwa kwa lengo la kupata magogo ya kujengea mashimo na wakati huo binadamu kufanya uchenjuaji bila kutumia vifaa kinga kunakosababisha madhara ya kiafya.

"Shirika la Afya Duniani (WHO) limeitaja zebaki kuwa ni miongoni mwa vyanzo 10 hatarishi kwa afya ya binadamu na kutokana na hali hii, Jumuiya ya kimataifa ilipitisha Mkataba wa Minamata mwaka 2013, wenye madhumuni ya kulinda afya ya binadamu dhidi ya madhara ya uchafuzi wa mazingira unaotokana na kemikali hiyo.

"Madhara makubwa ya kiafya yatokanayo na zebaki ni pamoja na kuathirika kwa mfumo wa neva, miguu na mikono kufa ganzi, kukosa nguvu, misuli kulegea, figo kuathirika, uono hafifu, kupoteza uwezo wa kusikia na kuongea, mimba kuharibika, kuzaa watoto wenye ulemavu wa akili, kupoteza kumbukumbu, kukosa usingizi kwa muda mrefu na kiharusi," alisema. Aliongeza kuwa katika kuhakikisha wanalinda afya ya binadamu dhidi ya madhara yatokanayo na zebaki, Tanzania ilishiriki kikamilifu katika majadiliano ya kuanzishwa kwa Mkataba wa Minamata na kutia saini makubaliano yao mwaka 2013 na kuuridhia mwaka 2020.

Kwa mujibu wa ibara ya saba ya Mkataba wa Minamata inazielekeza nchi wanachama kupunguza au kusitisha kabisa matumizi ya zebaki.

Tanzania ilitekeleza mradi wa miaka miwili wa kuandaa Mpango Kazi wa Taifa wa Miaka Mitano (2020-25) wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki.

Nyamanga alisema mradi huo ni nyenzo mojawapo ya kupunguza na iwapo itawezekana kuondosha kabisa matumizi ya zebaki katika shughuli za uchimbaji mdogo wa dhahabu kwa kuhamasisha matumizi ya teknolojia mbadala ili kulinda afya ya binadamu na mazingira kwa ujumla.

# Wasiochanja mifugo yao waonywa Bariadi

Na Happy Severine, BARIADI

KAIMU Ofisa Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi, Magdalena Gwandu, amesema wananchi wasiojitokeza kwa hiari kuchanja mifugo yao watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria zinazoongoza Sekta ya Mifugo.

Gwandu alisema hayo jana wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika kwenye Ukumbi wa Bariadi Motel mjini Bariadi.

Alisema wananchi ni lazima watambue kuwa kuchanja mifugo chanjo za magonjwa mbalimbali ni lazima na si hiari na atakayekiuka atachukuliwa hatua za kisheria.

Kaimu Ofisa Mifugo huyo alisema kwa kipindi cha miezi sita (Oktoba hadi Machi) wamechanja mifugo 300 kati ya mifugo 8000 iliyopo ndani ya halmashauri hiyo, idadi ambayo ni kidogo.

Alisema uchanjaji wa mifugo haukufikia lengo walilojiwekea la kuchanja nusu ya mifugo yote iliyokuwapo kutokana na mwitikio mdogo wa wananchi ambao wamekuwa wagumu na wabishi kupeleka mifugo yao kuchanjwa.

Aliongeza kuwa tayari wameshatoa elimu juu ya umuhimu wa chanjo kwa mifugo na wanaendelea kutoa elimu ili wachanje idadi kubwa ya mifugo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi, Elias Masanja, aliagiza idara ya mifugo kuendelea kutoa elimu ya chanjo ili wananchi wengi wajitokeze kuchanja mifugo yao.

Alisema mbali na chanjo za mbuzi, ng'ombe, kondoo na kuku, pia waendelee kutoa chanjo kwa mbwa na kuwaua wale wanaozagaa mitaani.

Baadhi ya madiwani walisema kumekuwa na kero ya mbwa wengi wanaozagaa ovyo mitaani na kusababisha madhara kwa binadamu, hasa watoto wadogo.

Walisema mbwa wengi walioko mitaani hawajachanjwa na pindi wanapong'ata binadamu wanasababisha madhara makubwa na kuiomba serikali kupitia idara hiyo kudhibiti tatizo hilo kwa kuwaua mbwa wote 'wasioeleweka mitaani'.

"'Ni vyema zoezi la uchanjaji mbwa liwe endelevu ili kuweka kinga kwa wananchi wetu wanaoathirika kupitia mbwa na pia wafanye msako wa kuwaua mbwa wote wa mitaani," Robert Rweyo, Diwani wa Somanda, alisema.

Juma Musa, mkazi wa Bariadi, alishauri elimu zaidi itolewe ili wananchi wajue faida za kuchanja mifugo yao.

## Ukiwaona watoto hawa, toa taarifa

**Na Mwandishi Wetu**

MTOTO Glory Martin (5) anadaiwa kupotea katika mazingira ya kutatanisha eneo la Gongolamboto jijini Dar es Salaam.

Baba wa mtoto huyo, Martin Ndube, akizungumza na Nipashe jana, alisema mtoto wake alikwenda kanisani na kaka yake eneo la Majumbasita Ukonga mwishoni mwa wiki, lakini hakurudi nyumbani.

"Tumemtafuta maeneo mbalimbali hatujampata. Tunaomba mtu yeyote atakayemwona atoe taarifa kituo cha polisi chochote au apige simu 0718/551470 au 0655/636204," alisema.

Baba huyo alisema ameshatoa taarifa Kituo cha Polisi Stakishari na kufungua jalada namba STK/RB/2685/2022.

Vilevile, mtoto Happiness Mstafa (12) anadaiwa kupotea eneo la Bunju B mkoani Dar es Salaam.

Mama mzazi wa mtoto huyo, Leah Filipo, alidai katika mazungumzo na Nipashe jana kuwa mwanawe alipotea mwishoni mwa wiki baada ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani kisha kuondoka.

"Alikwenda shuleni, aliporudi hakunikuta nyumbani, alibadilisha nguo na kuondoka hadi leo hajarudi. Tumemtafuta kila sehemu hatujamwona. Yeyote atakayemwona atoe taarifa kituo cha polisi au apige simu 0685/741962 au 0672/115923," alisema.

Mama huyo alisema ameshatoa taarifa Kituo cha Polisi Mabwepande na kufungua jalada MBD/RB/724/2021.


Happiness Mstafa


Glory Martin

# Jukwaa wanawake Kiwanda Sukari Kilombero lazinduliwa

● WAHAMASISHA CHANJO YA CORONA

**Na Mary Geofrey**

KATIKA kuadhinmisha Siku ya Wanawake Duniani, wanawake kutoka Kampuni ya Sukari Kilombero wamezindua rasmi Jukwaa la Wanawake ikiwa ni hitimisho la shughuli mbalimbali zilizofanyika katika wiki nzima ya maadhimisho hayo.

Uzinduzi huo ulifanyika mwishoni mwa wiki, mgeni maalumu akiwa Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Hanji Godigodi, na kushuhudiwa na watendaji wa serikali katika ngazi mbalimbali pamoja na wakuu wa idara kutoka kwenye kampuni hiyo ya sukari.

Katika hotuba yake, Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Godigodi, aliipongeza kamati ya maandallizi ya uzinduzi wa jukwaa hilo iliyoongozwa na Willa Haonga kwa kuja na wazo hilo ambalo lengo lake ni kuwainua wanawake kwa kuwajengea uwezo, kuwapa motisha ya kujiamini na kutatua vikwazo vya kijinsia.

Aliupongeza uongozi wa kampuni kwa kuidhinisha uundwaji wa jukwaa hilo ambalo litabadilisha taswira nzima ya kampuni na kuifanya kuwa endelevu kwa kujali usawa wa kijinsia mahala pa kazi.

Akifungua rasmi jukwaa hilo, mgeni rasmi katika uzinduzi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Sukari Kilombero, Guy Williams, alipongeza kamati ya maandalizi kwa kufanikisha uzinduzi huo pamoja na shughuli mbalimbali zilizofanyika katika wiki nzima.

Mkurugenzi huyo alisema kampuni ina mikakati zaidi ya kufanya maboresho mengine mbalimbali katika kukuza usawa wa kijinsia na kumwezesha mwanamke.

"Mbali na kukemea vitendo vya unyanyasaji na kunyayapaa wanawake mahala pa kazi na majumbani, kampuni imedhamiria kukuza ushiriki wa wanawake katika uamuzi na shughuli za kampuni ikiwamo kuongeza idadi ya wanawake katika ajira na nafasi za uongozi.

"Hili litawezekana kwa kuwajengea wanawake uwezo wa kujiamini na kujithamini kupitia fursa za mafunzo na kuwapa muda wa kujiendeleza kielimu sambamba na kuweka mazingira wezeshi mahala pa kazi ili kukidhi mahitaji yao ya kijinsia pamoja na malezi," Williams alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Uzinduzi wa Jukwaa la Wanawake wa Kampuni ya Sukari Kilombero, Willa, aliushukuru uongozi wa kampuni hiyo kwa kuwawezesha wanawake wa kampuni hiyo kuungana na wanawake wengine ulimwenguni kote katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani.

Willa ambaye ni Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa Kampuni hiyo, alisema kuwa katika kuendana na kaulimbiu ya mwaka huu isemayo 'Usawa wa Kijinsia kwa Maendeleo Endelevu', wanawake walifanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo ikiwa ni pamoja na kufanya usafi wa mazingira na kupanda miti katika maeneo mbalimbali yanayozunguka kampuni.

Pia walihamasisha upimaji wa afya kwa wanawake na kupata chanjo ya UVIKO-19 pamoja na fursa ya kutembelea dawati la jinsia.

Jukwaa la wanawake katika Kampuni ya Sukari Kilombero limeanzishwa kwa lengo la kuwaendeleza wanawake na kuwajengea uwezo kiutendaji, kuandaa mkakati na mpango kazi jumuishi wa usawa wa kijinsia, kutatua kero mbalimbali za kijinsia na kudumisha utamaduni wa kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani kila mwaka kama chachu ya kujadiliana masuala mbalimbali yanayowahusu wanawake katika kampuni hiyo na jamii kwa ujumla.




Mkuu wa Wilaya ya Kilombero mkoani Morogoro, Hanji Godigodi (wapili kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Sukari Kilombero, Guy Williams, pamoja wakionyesha bango la uzinduzi wa uundwaji jukwaa la wanawake wa kiwanda hicho, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake TPA wawapa kadi za afya watoto 200

**Na Gwamaka Alipipi**

WANAWAKE wa Mamlaka ya Bandari (TPA) wametoa bima za afya kwa watoto 200 wilayani Temeke mkoani Dar es Salaam.

Kadi hizo zimetolewa kwa lengo la kuunga mkono jitihada za serikali za upatikanaji wa huduma za afya kwa wote.

Watoto hao ni wenye uhitaji maalumu kutoka familia duni ambazo hazina uwezo wa kumudu gharama za matibabu na hivyo katika wakati mgumu wanapougua.

Akikabidhi kadi hizo juzi wilayani Temeke, Kaimu Meneja Utumishi TPA, Mwajuma Mkonga, alisema fedha hizo zimepatikana baada ya wanawake hao kujichangisha ili kusaidia wenye uhitaji.

Meneja huyo alisema katika mwezi wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani wamewezesha kukatiwa bima ya afya watoto 400. Kati yao, 100 wa Ilala, 100 Kigamboni na 200 Temeke.

"Tunatambua mchango wa serikali katika kuboresha huduma za afya na kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora za matibabu.

"Katika kuunga mkono hili, wanawake wa Bandari tuliamua kwa hiari yetu kuchangishana fedha, pia kushirikiana na wadau wetu," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, alisema wilaya yake ina watoto wengi wanaohitaji msaada wa aina hiyo kwa kuwa wanatoka katika familia zenye kipato cha chini.

Jokate alisema Wilaya ya Temeke ina wananchi wengi ambao kipaumbele chao ni kutafuta riziki ya kila siku ili wapate kula, hivyo wapo wanaoshindwa kumudu gharama za matibabu.

"Mlichokifanya mmewatua wazazi mzigo wa kuwahangaikia watoto wanapohitaji matibabu.

Temeke tuna wananchi wengi na wengi wao hawana hali nzuri kiuchumi, hivyo kuwasaidia matibabu ya watoto ni jambo kubwa," alisifu.

Aliwasisitiza wazazi umuhimu wa kupata mapema vyeti vya kuzaliwa badala ya kusubiri muda ambao mtoto anahitajika kwenda shuleni kuanza masomo.

Meneja wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) Wilaya ya Temeke, Fortunata Raymon, alitoa wito kwa taasisi zingine kuguswa kusaidia watoto kutoka familia duni.

Fortunata alisema: "Tunaishukuru Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwa namna ambavyo tunashirikiana katika kuhakikisha wananchi wanapata bima ya afya.

"Niwapongeze wanawake hawa kwa kuamua kukumbuka afya ya mtoto, wangeweza kutumia fedha zao kwa matumizi mengine. Nitumie fursa hii kuwaomba wadau wengine kulitazama suala hili."

# Nape: Bunge lina uhuru kurusha matangazo 'live'

**Na Thobias Mwanakatwe,** ARUSHA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia na Habari, Nape Nnauye, amesema endapo Bunge litaamua kurusha matangazo yake 'live' hata kwa saa 24 serikali haitaliingilia kwasababu lina uhuru wa kufanya hivyo.

Alisema hayo juzi wakati akihojiwa kwenye kipindi cha Dakika 45 kinachorushwa na runinga ya ITV kila siku ya Jumatatu.

"Mimi niseme ni wajibu wa Bunge na wajibu wa wabunge na serikali hatuna mkono wetu, Bunge likiamua leo kwenda saa 24 hatuna tatizo hatutawaingilia ni wa Bunge wana studio yao, wana bajeti yao, wana utaratibu wao na wana uhuru wa kufanya," alisema.

Nnauye alitoa wito kwa wabunge wakati umefika wajadiliane kanuni za kuendesha studio yao, wakubaliane halafu waendelee.

Alisema kwenye mabunge yote ya Jumuiya za Madola mfano Afrika Kusini, Kenya na Uganda kila Bunge lina kanuni zake ya namna ya kurusha matangazo ya Bunge live.

"Kwa mfano usingetamani uonyeshe wabunge wako wanapigana ngumi, sasa mkiwa 'live hundred percent' yote ile itaonekana kwa hiyo yapo mambo ambayo wanayapunguza," alisema.

Nnauye alisema ni bahati mbaya baadhi ya watu wamekuwa wakisema yeye (Nape) ndiye alisababisha Bunge lisiwe linarushwa live kama ilivyokuwa awali.

"Kwa mujibu wa kanuni za utangazaji ambazo zilitungwa mimi nikiwa sio mbunge zilitungwa huko nyuma zinasema, Bunge la Tanzania ndilo litakalopanga matangazo yake ya kazi zake yarushwaje," alisema na kuongeza.

"Bunge sio serikali, sasa watu wanaposema ni Nape najua 'reference' yao ni kwamba wakati wa uamuzi wa Bunge kubadilisha namna ya kufanya matangazo yake watangazaji wakubwa wa Bunge ilikuwa TBC."

Nnauye alisema baada ya Bunge kuamua kutengeneza kanuni na studio yake kipindi hicho akiwa waziri waliamua kuiondoa TBC na TV zingine ili Bunge litengeneze mfumo wake.

Alisema hivi sasa Bunge lina studio yake na hata leo mtu haingii na kamera ndani badala yake matangazo yanachukuliwa kutoka kwenye studio yake.

"Mimi nilibeba dhamana sasa kwamba Nape ndiyo ametuondoa si kweli kabisa mimi sina mamlaka ya kwenda kuzuia Bunge lisirushwe live mamlaka hayo sina ni kanuni za bunge," alisema.

Nnauye alisema ni bahati nzuri kwamba Spika wa Bunge ameshasema wako tayari kufikiria namna bora ya kuboresha matangazo ya yakaaje na watashauriana na serikali.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Mark Ocitti (kushoto), akizungumza na wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kabla ya kuanza ziara ya kutembelea kiwanda cha SBL, mkoani Dar es Salaam jana, kuangalia jinsi mfumo wa stempu za kielektroniki unavyofanya kazi kiwandani hapo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## TRA yatakiwa kufungua ofisi Nyanghwale, Bukombe

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

KATIBU Mtendaji Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), Dk. Godwill Wanga, ameitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mkoa wa Geita kufungua ofisi ya TRA Wilaya ya Nyanghwale na Bukombe ili kuongeza ukusanyaji wa mapato ya serikali.

Alitoa rai hiyo jana wakati akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Biashara la mkoa huo kilichofanyika Halmashauri ya Mji wa Geita.

Alisema kutokuwa na ofisi za TRA katika wilaya hizo mapato mengi yanapotea na serikali inashindwa kupata mapato.

Aidha, alisema kuna changamoto nyingi katika Mkoa wa Geita ambazo ni umiliki wa ardhi, mambo ya madini, ardhi na usimamiaji wa utekelezaji wa maazimio.

Alisema changamoto kubwa ni ardhi, kwa sababu sehemu nyingi ya Mkoa wa Geita maeneo mengi hayajarasimishwa.

Alisema kuna vijiji 486, lakini vilivyorasimishwa ni 44 na wametoa maazimio ya kikao kwamba lazima vijiji vyote virasimishwe.

Alisema wapo watu wengi wanafanya biashara, lakini hawajarasimishwa, na azimio ni kwamba lazima wafanyabiashara wote waingizwe kwenye mpango huo. Pia machinga yeyote ambaye hatafanyia eneo lililotengwa na serikali atakuwa anajitafutia matatizo.

Vile vile, alisema maeneo yote yaliyotengwa kwa ajili ya wamachinga miundombinu iwe bora na iwekwe sawa ili waweze kufanya biashara yao salama. Kwa sababu kuna maeneo mengine miundombinu sio salama.

"Tutafanya tena mkutano wa kutathmini mambo yote tuliyokubaliana kikao kijacho ambacho kitafanyika Juni 10, mwaka huu kwa ajili ya kuangalia kama mambo yote yametekelezwa," alisema Dk. Godwill Wanga.

# Maofisa ugani kununuliwa pikipiki 2,000

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI kupitia Wizara ya Kilimo, inakusudia kuwanunulia pikipiki 2,000 na vifaa vya kazi vikiwamo vya kupimia afya ya udongo 143 maofisa ugani nchini ili waweze kutoa huduma bora katika mashamba ya wakulima.

Akifungua mafunzo ya shamba darasa kwa maofisa ugani kutoka mikoa sita kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, mwakilishi wake kutoka wizara hiyo, Charles Mjema, alisema pikipiki hizo zitanunuliwa baada ya ongezeko la bajeti ya mwaka 2021/22 kwa ajili ya kutoa huduma za ugani kutoka Sh. milioni 600 hadi Sh. bilioni 11 fedha ambazo zitatumika kwa ajili ya mafunzo.

Alisema serikali imedhamiria maofisa ugani hao kuchangia kuleta tija katika kilimo kwa kuhakikisha wanatoa elimu ya kilimo bora katika mashamba ya wakulima ili waweze kujua afya ya udongo na kuepuka kuharibu udongo na kupunguza uzalishaji.

Alisema uzalishaji wa mazao nchini unafanywa kwa mazoea na wakulima wengi hawatumii kanuni bora za kilimo jambo linalosababisha kuwa na uzalishaji mdogo na serikali imedhamiria katika msimu huu wa kilimo 2021/22 kuanza kuwekeza rasilimali hizo. Alisema kwa kuanzia serikali itaanza na mikoa mitatu ya kielelezo ikiwamo Dodoma, Singida na Simiyu na uzoefu utakaopatikana utasaidia kutengeneza mpango wa kitaifa wa kuimarisha huduma za ugani katika mikoa mingine iliyobaki.

Kwa upande wake mratibu wa mradi wa kujenga uwezo katika mikataba ya Kimataifa ya Mazingira, unaosimamiwa na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO), Diomedes Kalisa, alisema tayari wamependekeza kuondolewa sokoni aina 24 za viuatilifu ambavyo sio rafiki wa mazingira vinavyotumika katika kilimo.

Alisema FAO kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu vya Kudhibiti Visumbufu (TPRI), wamependekeza kuvifutia usajili viuatilifu hivyo kutokana na kusababisha upotevu wa baionuwai na kutishia usalama wa chakula.

Alisema badala yake FAO imekuja na mbinu mbadala ikiwamo mashamba darasa na kutumia kemikali rafiki kwa mazingira zitakazotumika katika kilimo na kuokoa bainowai ikiwamo nyuki wanaotumika kuchavusha mazao mbalimbali.

Kalisa alisema viuatilifu hivyo pia vimependekezwa kutolewa kwa sababu vinasababisha saratani, vinakaa sana kwenye mazingira, vinakuwa na sumu kali kwa viumbe hai na kutishia uwapo wa usalama wa chakula hapa nchini.

Alisema mradi huo unaofadhiliwa na Umoja wa Nchi za Ulaya (EU), utatekelezwa katika Wilaya za Kilosa, Mbalari, Same, Kigamboni, Karatu na Kilolo utahusisha zaidi katika sekta ya kilimo kuangalia namna ya kupunguza kupotea kwa baionuwai hiyo.

Naye Ofisa Mazingira wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu, Ally Mdangaya, alisema wakulima wa wilaya hiyo wamekuwa na imani kuwa hawawezi kupata mazao bila kutumia kemikali, lakini hivi sasa wameshaanza kupatiwa elimu ya kuachana na kemikali hizo na badala yake watumie njia ya kibaiolojia ambayo ni rafiki wa mazingira.



Ukurasa 12

MWAKA 1 WA RAIS SAMIA

## Ngawaiya; ameonyesha ukomavu kisiasa, pia anaujali utawala bora




Ukurasa 13

## Afrika na kazi ya kutazama upya misingi ya mtangamano



Ukurasa 14

## Wanawake tisa wanaoshikilia wizara, kikosi kazi anachojivunia Rais Samia


# siasa

JUMATANO MACHI 16, 2022

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe


DK. MAYROSE MAJINGE

# Aliyeomba ateuliwe urais bendera CHADEMA aja upya 'Samia atosha'

- Sababu; ametathmini amesheheni
- Rai yake; anapaswa aungwe mkono

**Na Romana Mallya**

UNAPOONA mpinzani hasa wa kambi tofauti ya kisiasa, anapongeza kazi zinazofanywa na mshindani wake, iko bayana kubebea tafsiri nyingi. Lakini, kubwa inamaanisha kuwa "unatosha' kwenye nafasi yako."

Mantiki hiyo inabeba uhalisia wake kutoka kwa aliyeshika nafasi ya tatu katika mchujo wa kumpata mgombea urais kuelekea Uchaguzi Mkuu nchini uliopita wa mwaka 2020, kupitia bendera ya chama - CHADEMA, Dk. Mayrose Majinge.

Mwanamama huyo, hafichi mantiki yake alipohojiwa na Nipashe wiki iliyopita, akiainisha kufurahishwa na kazi kubwa anayoifanya Rais Samia, ndani ya mwaka mmoja wa uongozi wake unatimu Jumamosi wiki hii.

Hiyo ni tangu apishwe kuongoza nchi, baada ya kifo cha mtangulizi wake, Dk. John Magufuli, aliyefariki dunia Machi 17, 202.

Tukio hilo linaweka rekodi kushika wadhifa huo wa kwanza kwa mwanamama wa Afrika Mashariki kutimu siku ya 365, hitimisho lake likitarajiwa kuendana na ukataji keki kwa kuwatumika Watanzania kwa nafasi hiyo.

Dk. Mayrose ambaye kitaaluma, pia ni mbobezi katika masuala ya watu na maendeleo, anashauri sasa ni wakati mwafaka wa kumpenda na kumtia moyo, Rais Samia, katika yale atakayoendelea kuitimiza katika kipindi cha utawala wake.

Anaeleza, anashindwa kuzizuia hisia zake kwa Rais Samia akiwa na ufafanuzi: "Watanzania wenzangu, kwa kuwa imempendeza Mungu akatufungulia ukurasa mpya wa kuwa na kiongozi mkuu mwanamke katika nchi yetu kwa mara ya kwanza."



Dk. Mayrose Majinge. **PICHA: MAKTABA**

"Ninaomba sana tuutumie ukurasa huu mpya kujitafakari kila mmoja wetu na kujipanga upya hasa kifikra ili tufurahie kwa kuwa na taifa ambalo ni zuri na bora."

Dk. Mayrose anaendelea: "Taifa ni watu tukiwa ubora na ubora wa watu ambao wanawaza mambo mazuri na kufanya mambo mazuri na kufikiria mambo mazuri, wanaoshirikiana, wanaodhaminiana na kutiana moyo taifa litasonga mbele."

Mwanasiasa huyo msomi, anafafanua kupitia lugha ya kifalsafa, kwamba ili jamii iweze kuwa na maisha bora, inatarajiwa kuwa makini, ikianzia namna wanavyofikiri.

"Tuwe makini kwa kauli zetu, maana maisha bora yanatokana na jamii bora. Hatuwezi kujenga jamii bora kama tuna tabia ya kushushana, kubezana kudharauliana na kudhalilishana wakati mwingine," anaeleza.

Anasema kwa muda mrefu kumekuwapo na hulka kwenye tabia za kubeza na kuwa na ari ya kusubiri mambo kutokea kwa wengine hasa wanaofanya jambo jipya au aliyepata nafasi fulani ambayo hawakuwahi kuwa nayo awali.

"Mfano mmoja ni wakati Rais Samia anaingia madarakani, ukweli ni kwamba hakuna aliyetarajia. Wapo waliosema hataweza eti kwa sababu ni mwanamke.

"Tabia ya kudhaniana mabaya imekuwapo katika jamii yetu kwa muda mrefu sasa. Hivyo, imekuwa inasababisha kufifisha umoja na kudumisha unafiki. Ni mambo mabaya yanayochangia kurudisha nyuma maendeleo yetu," anafafanua.

Mama huyo anawakumbusha Watanzania ili waweze kuwa na maisha bora, lazima wawe makini na fikra zao, pia kauli wanazotoa.

"Maana maisha bora hutokana na jamii bora. Hatuwezi kujenga jamii bora, kama tuna tabia ya kushushana, kubezana, kudhalilishana...." anasisitiza.

Msomi Dk. Mayrose, anadokeza anachokiita kitaalamu 'sheria ya mvuto' kwamba ni falsafa inayopendekeza mawazo bora katika maisha ya mtu na mawazo hasi huleta matokeo mabaya, hivyo siyo sahihi kuchukua au kuishi na fikra potofu.

Anafafanua kwamba, mtu anapofanya hivyo, anaangukia katika kujipunguzia imani na upendo kwa wengine.

"Imani na upendo vikipungua, ni wazi hutakuwa karibu na huyo mtu. Kwa kukaa mbali naye, utajikuta unakosa yale mazuri aliyonayo, ni muhimu kukumbuka kwamba hapa duniani hakuna aliyemkamilifu.

"Kila mtu ana mapungufu yake. Hata wewe mwenyewe unayo mabaya mengi, ndiyo maana wabobezi wa maendeleo ya watu

INAENDELEA UK. 13

# Ngawaiya; ameonyesha ukomavu kisiasa, pia anaujali utawala bora

• Aorodhesha matukio ya mfano wa kuigwa



Mwenyekiti wa CEGODETA, Thomsa Ngawaiya, alipozugumza na wanahabari wiki iliyopita, Kulia kwake ni mdau mwingine wa asasi hiyo, Hamad Tao. **PICHA: SABATO KASIKA**

**Na Sabato Kasika**

WIKI hii ndio kilele cha mwaka mmoja kuhitimu tangu aingie madarakani, jana Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye kabla ya hapo alikuwa Makamu wa Rais, alipokula kiapo kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na sasa anatimiza mwaka mmoja madarakani.

Yapo mengi ambayo ameyafanya kwa maendeleo ya nchi, huku akionekana katika mambo anuai kuanzia uzungumzaji, anavyofikisha ujumbe, uungwana na mengine mengi madogo.

Inaelezwa kuwa kitendo chake cha kukutana na viongozi wa chama kikuu cha upinzani cha CHADEMA na kufanya nao mazungumzo ndani na nje ya nchi, kimeonyesha ishara ya ukomavu wa kisiasa.

Ni hatua inayoelezwa kuwa ni taswira yake chanya katika uongozi wake ndani ya mwaka mmoja madarakani, ambayo inapaswa kuungwa mkono na wapenda demokrasia na utawala bora.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, anakitaja kuwa kitendo kinachoonyesha anavyoutafsiri ma kuutambua upinzani si uadui, bali ni hali ya utofauti kiitikadi. Lakini mustakabali wa kujenga nchi ubaaki palepale ni wa wote.

Ngawaiya, aliyewahi kuwa mbunge na kiongozi wa ngazi ya juu katika kambi ya upinzani katika chama cha TLP, kabla ya kurejea chama tawala - CCM, amewaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam wiki hii, akitoa tathmini ya mwaka mmoja ya CEGODETA kuhusu nafasi ya mwaka mmoja wa Rais Samia madarakani.

> Ilikuwa ni baada ya serikali kutoendelea na kesi iliyokuwa ikimkabili na wenzake watatu. Hatua hizo zote zimeonyesha ni jinsi gani anajali utawala bora na amekomaa kisiasa, anajua kuwa upinzani si uadui.



Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: MTANDAO**

### UKOMAVU KISIASA

Ngawaiya anaeleza kwamba utawala bora umejengwa katika ushirikishwaji, maridhiano na utumiaji wake wa madaraka umeenda sambamba na ushirikishwaji wa wanaoongozwa, kuhakikisha shughuli za umma zinaendeshwa kwa mawazo na maslahi ya wengi.

"Suala la kuongoza ni kwamba, ni mawazo ya wote bila kujali itikadi za vyama vya siasa, yanahitajika na hilo Rais analifanya. Ndiyo maana amekutana na viongozi wa chama kikuu cha upinzani cha CHADEMA," anasema Ngawaiya.

Anarejea tukio la Rais kuwa ziarani katika nchi za Ulaya alikokutana na Tundu Lissu, aliyekuwa mshindani kwenye mbio za kuwania urais mwaka 2020, pia Makamu Mwenyekiti wa chama hicho kufanya wa sasa, walipofanya mazungumzo mwezi huu amekutana na Mwenyekiti wake, Freeman Mbowe Ikulu, Dar es Salaam, muda mfupi baada ya kutoka gerezani.

"Ilikuwa ni baada ya serikali kutoendelea na kesi iliyokuwa ikimkabili na wenzake watatu. Hatua hizo zote zimeonyesha ni jinsi gani anajali utawala bora na amekomaa kisiasa, anajua kuwa upinzani si uadui," anasema Ngawaiya.

Pia mkuu huyo wa CEGoDETA anafafanua, katika mwaka mmoja madarakani, Rais Samia ameonyesha uvumilivu na mwenye kufanya uamuzi kupitia kusikiliza kila mmoja.

Hapo anamwongezea ushauri wa kukutana na makundi mengi zaidi ya wanasiasa, asasi za kiraia na watu wa kada mbalimbali, ili kupata mawazo na maoni mengi ya kumsaidia kuongoza taifa.

"Kama nilivyosema kuwa katika mwaka mmoja madarakani, ameonyesha ni jinsi gani alivyo mvumilivu na mwenye kufanya maamuzi kupitia kusikiliza kila mmoja na si kuamua mambo kwa pupa au kuonea mtu, tunamshauri akutane na makundi mengine zaidi kujadiliana nayo," anasema.

### MBALI NA UONEVU

"Ndani ya mwaka mmoja, Rais Samia ameonyesha ni jinsi gani asivyopenda watu waonewe kubambikiwa kesi na kupelekwa mahakamani kwa makosa ambayo matokeo yake huwa ni kuachia watu huru," anasema.

"Kama... mtakuwa mnafuatilia utendaji wake, mtakuwa mnajua jinsi alivyoiagiza TAKUKURU kufuta kesi mbalimbali ambazo ushahidi wake ulikuwa haueleweki na bado anaendelea kufanya hivyo," anasema.

Ni kauli iliyoendana na kuachiwa huru jamii ya kada mbalimbali, wakiwamo viongozi wa dini, ambayo Mwenyekiti wa CEGODETA anaifafanua: "Hivi karibuni kama mnakumbuka, kutokea tuhuma za mauaji zinazohusu polisi...aliagiza kuundwa kamati huru ya kuchunguza tuhuma hizo badala ya polisi kujichunguza."

Ngawaiya anataja namna hiyo, ni sehemu ya yaliyo muhimu katika kuzingatiwa utalawa bora ambao msingi wake ni haki na haitakiwi kumwonea mtu, bali kila mmoja apate haki kulingana na matendo yake.

Anaongeza kwamba katika mwaka wake mmoja madarakani, Rais Samia ameonyesha namna ya kusimamia uwekaji mbali mfumo dume katika uongozi, akitambua suala la uongozi ni kuwatumikia wananchi kwa manufaa ya taifa pasipo kujali ni mwanaume au mwanamke, muhimu kwake ni usawa kwa mwanadmu.

Anataja Rais Samia anasimamia na kuendeleza miradi ya kimkakati inayolenga kufanikisha utekelezaji Sera ya Viwanda hususan kupitia miradi ya nishati ya umeme, iliyoanzishwa na mtangulizi wake, Dk. Magufuli.

Anafafanua kuwa Dk. Magufuli aliweka kipaumbele cha kusimamia utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme wa Nyerere katika Mto Rufiji (Stiegler's Gorge), kwa lengo la kufikia uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

"Hata Rais Samia alipoingia madarakani, aliahidi kuendeleza miradi ya mtangulizi wake ikiwamo pia ya ujenzi wa barabara na mingine ambayo tunaona ikiendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali," anasema.

# Afrika na kazi ya kutazama upya misingi ya mtangamano

**Na Michael Eneza**

MIJADALA kuhusu umoja wa Afrika au umoja wa Waafrika duniani umekuwapo majukwaani tangu mwaka 1945, ulipofanyika mkutano wa tano wa Ujumuishaji wa Waafrika Duniani (Pan-Africanist Conference) jijini Manchester huko Uingereza.

Mikutano iliyotangulia ilijumuisha zaidi jamii za Kiafrika zilizotokana na biashara ya watumwa kupitia Bahari ya Atlantiki, iliyoendelea kwa miaka 300. Ilianza mwaka 1519 hadi 1848. Mwaka 1519 ndiyo mtumwa wa kwanza alishushwa pwani ya Florida nchini Marekani, Uingereza ikapiga marufuku biashara ya utumwa 1807 na Ufaransa ikajivuta hadi 1848 ndipo ikashindwa kuendelea na biashara hiyo.

Yako matukio kadhaa hivi karibuni yaliyoleta mjadala huo kwa mara nyingine miongoni mwa wanaharakati na vyombo vya habari.

Ikiwamo kuanza kuratibiwa kwa Ukanda wa Biashara Huria Afrika (AfCFTA) ambao umeweka misingi ya mapendekezo ya siku nyingi ya kuundwa Umoja wa Kiuchumi wa Ulaya na Afrika (EPA).

Wakuu wa nchi wa pande hizo mbili walikuwa Brussels, Ubelgiji makao makuu ya Umoja wa Ulaya (EU) majuzi kuratibu hatua mpya za kufikiwa kwa lengo hilo ni kuwaunganisha Waafrika ila kupitia kwa Wazungu?

Mjadala wa Idhaa ya redio kimataifa ulijaribu kutanzua kama bado upo uwezekano wa kuwaunganisha watu wa Afrika, au nchi za Kiafrika wao wenyewe na siyo kupitia jumuiya tofauti na nchi za Ulaya.

Kuna Jumuiya ya Madola, na ile ya wenye ushirika na lugha, utamaduni wa Ufaransa 'Francophone' pia lipo kundi la nchi zenye lugha ya Kireno, ila hazina ujumisho halisi hujiita Lusophone.

Baadhi ziko katika Jumuiya ya Madola au 'Francophonie.' Ukanda uliobaki ni wa nchi za Kiarabu Afrika Kaskazini, lakini hata Comoro ni mwanachama, nazo pia zina uhusiano na zile zinazozungumza Kifaransa kwa baadhi yao na siyo wakereketwa wa kujijumuisha na Ufaransa.

Ukifanya uchambuzi wa karibu unakuta kuwa wanacholilia wasomi wa Kiafrika hata katika mabara mengine hakipo, kuwa maeneo makubwa kama mabara yanganishwe na utaifa au rangi ambayo Afrika inazua utaifa mpana wa Waafrika.

Kuna Jumuiya ya Uarabu ambayo msingi wake ni lugha moja ya Kiarabu, wakati Afrika haina jumuiya ambayo msingi wake ni lugha ya ndani ya Afrika na lugha hizo ni chanzo cha ukabila na vita vya ndani badala ya uzalendo wa ngazi ya kimataifa wasomi wanaoulilia.

Mjadala redioni unazitaka nchi za Afrika zijenge umoja wa peke yao na si kutanguliza umoja na Ulaya, ziunganishwe na Kiswahili au Kihausa, kwa mfano.

Ni wazo ambalo lingehitaji himaya kubwa ya Kiswahili au Kihausa kabla ya ukoloni, iwe ndiyo msingi wa dola baada ya uhuru, mradi huo haukuwapo kabla hauwezi kuundwa karne moja baadaye.

Barani Asia hakuna ujumuishaji wa Kiasia, au wa Kichina, Kibuddha, Kijapani au 'umajumui' wa aina nyingine, kutumia neno linalopendwa na baadhi ya wanaharakati kutafsiri 'Pan-Africanism' mara kadhaa.

Zipo jumuiya za kibiashara ambazo msingi wake ni mahusiano na Marekani au China katika nyakati tofauti, na ushiriki wa mifungamano ya ulinzi kwa mfano dhidi ya China hivi sasa, kuunganisha Australia, Japan, India na Marekani. Siyo 'umajumui' wa aina yoyote ila ulinzi.

> Mjadala redioni unazitaka nchi za Afrika zijenge umoja wa peke yao na si kutanguliza umoja na Ulaya, ziunganishwe na Kiswahili au Kihausa, kwa mfano.

Labda cha kusisitiza hapa ni kuwa muda wenyewe wa 'Pan-Africanism' sasa umekwisha, kwani dunia ina ajenda moja hivi sasa, ya demokrasia na utandawazi (ambao ni mhimili wa maendeleo kwa msingi wa mawasiliano, fursa na uhuru).

Licha ya kwamba mjadala redioni unagawanyika kati ya wanaosisisitiza Uafrika kama msingi wa ujumuishaji nchi au jamii za Afrika kwa jumla na wanaotoa hoja kuwa bila demokrasia, utawala wa sheria, kuondolewa udhalimu, ujumuishaji huo utakuwa ni mfumo wa kulinda tawala za kiimla, na siyo mwendelezo wa uhuru wa raia kama Ulaya.

Hapo ndipo hoja ilipo kuwa kama tunu za uhuru wa mtu binafsi na utawala wa sheria vinahakikisha utangamano kijamii na fursa kimataifa, 'umajumui wa Kiafrika' unaongeza nini?



Ujumbe wa Tanzania ulipohudhuria Mkutano wa Umoja wa Afrika (AU), jijini Addis Ababa, Ethiopia. **PICHA: MTANDAO**

## Aliyeomba ateuliwe urais bendera CHADEMA aja upya 'Samia atosha'

**INATOKA UK. 11**

wanasisitiza watu kuishi kwa kufuata kanuni ya dhahabu, ili kuweza kusimamia vema sheria ya mvuto," anaeleza.

Mgombea huyo, anatetea mtazamo wake kwamba wa Rais Samia kuwa rais, kwamba "imempendeza Mungu na kuwafungulia Watanzania ukurasa mpya wa kuwa na kiongozi mkuu mwanamke kwa mara ya kwanza, hawana budi wautumie kujitafakari.

"Tujitafakari kila mmoja kujipanga upya hasa kifikra ili tufurahie maisha kwa kufanya taifa letu kuwa mahali pazuri pa kuishi na kufurahi.

"Hii itawezekana ikiwa tu kila mmoja atatambua mazuri ya mwenzake na kuyatumia ipasavyo. Wabobezi wa masuala ya maendeleo ya watu wanashauri jamii kuishi maisha bora kwa kuzingatia matumizi bora ya sheria ya mvuto ikisimamiwa na kanuni ya dhahabu."

Anasema matumizi bora ya 'sheria ya mvuto' ikisimamiwa na 'kanuni ya dhahabu' Watanzania wataondokana na fikra potofu, kutiliana shaka, kuogopana, kunyosheana vidole, kulaumiana, kuchukiana kwa kigezo cha kujumuisha mambo, kuishi kwa hisia hasi na kutengana.

Pia anafafanua kwamba, iwapo jamii inaweka kando mabaya na wataachana na mambo kama hayo Watanzania wataweza kunufaika na karama au vipaji walivyopewa na Mungu.

Anasema jamii kuishi kanuni ya matumaini na suluhisho lake ni kupiga hatua katika matumizi bora ya sheria za mvuto, hata kuwafanya wasikate tamaa.

Anatol mfano wa glasi yenye maji nusu na kueleza kuwa mtu akiishika na kuuliza kundi la watu wanaionaje wapo watakaosema wanaona nusu tupu na wapo watakaojibu wanaona nusu imejaa.

"Kwa masikitiko ni kuwa jamii yetu imejaa watu ambao huwa ni mabingwa wa kuona mambo mabaya zaidi kuliko mazuri, tunakosa matumaini kwa wenzetu, tunawasema vibaya, tunawadharau, tunawachukia tunapoteza mazuri yao na hivyo tunaondoa thamani yao.

"Kwa kufanya hivyo, tunajikuta tunapoteza faida ambayo tungeipata kutoka kwao na hivyo tunapunguza tija ya maisha yetu."

DK. Mayrose anamtaka kila Mtanzania atafakari namna anavyowachukia wenzake na kutaka wasiwahesabie mabaya, bali watgemee mazuri, akifafanua: "Mti unaouchukia, huwezi kula matunda yake, maana hautautunza na kusababisha ukauke bila ya kuzaa matunda."

Mwanasiasa huyo anasema Watanzania wanapoutafakari mwaka mmoja Rais Samia kuwa madarakani, ni lazima kila mmoja atumie muda kujitafakari iwapo wanaishi kwa matumaini au kukata tamaa.

"Tunamwangalia Rais Samia kama glasi yenye nusu ujazo? Au nusu tupu? Ombi langu kwa Mungu atujalie kupenda kuona mazuri kwa wenzetu na hivyo atujalie na uwezo wa kumwangalia Rais Samia kwa matumaini makubwa ili tuweze kunufaika na mazuri yake ambayo ni mengi, tukiamua tunaweza."

# Wanawake tisa wanaoshikilia wizara, kikosi kazi anachojivunia

**Na Sabato Kasika**

SASA anatimiza mwaka mmoja katika utumishi wake wa umma, kwa wadhifa mkuu wa nchi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan. Uzoefu una safari ndefu, ila kwa dodoso fupi, alichonacho kitaaluma, zao la kilichokuwa Chuo cha Maendeleo ya Uongozi (IDM) Mzumbe (sasa Chuo Kikuu Mzumbe) maarifa ya uongozi yakiongezwa na darasa la ziada kiwango cha Uzamili.

Pia, kuna uzoefu wa kazi kuanzia kiwango cha kutumikia jamii, hata akalitumia taifa kwa mengi, ushuhuda mmojawapo ni kusaidia kuendesha usukani wa Bunge Maalumu la Katiba, jijini Dodoma, hapana shaka hadi kufika gari analoliendesha leo, analimudu.

Huyu ndiye Rais Samia Suluhu Hassan, lakini wengi hawapendi kumweka mbali na hadhi ya mama, hata akajulikana zaidi kwa 'aka' Mama Samia, katika awamu ya kwanza ya safari yake kuzitafuta siku 365 na robo, zinazotimia siku ya Jumamosi inayotusubiri.

Naam! Nirejee kidogo kwa wanamisemo, huyu ni mama na kama anang'ara, ujue wapo wa - mama wengi wanaofanikisha. Na kama yeye ni Rais, hapana shaka nyuma yake kuna kikosi kazi cha kwanza kinachomnyooshea njia, kwa jina kisiasa au kiutawala, hao ni baraza la mawaziri, ambao ndani yao ukipepesa macho, unawakuta kinamama tisa 'wa kazi', wajuzi na wenye maarifa, maprofesa kwa madaktari na uzoefu tele.

Hebu nikumegee hicho kikosi kazi cha kinamama kinachomnyooshea njia: Balozi Liberata Mulamula; huyo anashikilia Wizara ya Mambo ya Nje, akiwa mwanadiplomasia mbobezi, aliyetumikia balozi za Tanzania nchini Marekani na Mexico pia kabla ya hapo ana nasaba ya kazi hizo, Umoja wa Mataifa na Canada.

Hali kadhalika ameshahudumu kwa nafasi ya Katibu Mtendaji wa Mkutano wa Kimataifa wa Kanda ya Maziwa Makuu ya Afrika. Darasani ana Shahada ya Uzamili katika Siasa kutoka Chuo Kikuu cha St. John's, New York na ya kwanza aliipata katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Jenista Mhagama ni Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora: kitaaluma ni mwalimu, ngazi ya Stashahada akiwa mzoefu katika baraza la mawaziri, dalili za ufanisi wake zikimfanya ateuliwe kwa awamu kadhaa.

Mwalimu mwingine ni, Profesa Joyce Ndalichako; mwanazuoni mwandamizi katika taaluma ya ualimu, akizamia zaidi katika Tathmini ya Elimu, ambako mzizi wa utumishi wake wa muda mrefu, uko katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kabla ya kuteliwa kuwa Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA).

Baada ya hapo, Profesa Ndalichako, ambaye shahada yake ya kwanza ni ya ualimu wa hisabati, aliteuliwa kuwa mbunge na Waziri anayetumikia Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi katika awamu iliyopita, na awamu hii aligombea ubunge akashinda, kisha akadumu katika nafasi ya uteuzi ya waziri, sasa akitumikia Wizara inayohusika na kazi.



Rais Samia alipokula kiapo kuwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. **PICHA: MTANDAO**

> Dk. Hazara Pindi Chana; ni sura mpya katika safu ya baraza la mawaziri lililopo sasa, akiwa mbunge wa kuteuliwa anatumikia Sera, Bunge na Uratibu, katika Ofisi ya Waziri Mkuu.



Dk. Hazara Pindi Chana



Ummy Mwalimu



Dk. Stergomena Lawrence Tax

Dk. Hazara Pindi Chana; ni sura mpya katika safu ya baraza la mawaziri lililopo sasa, akiwa mbunge wa kuteuliwa anatumikia Sera, Bunge na Uratibu, katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

Ummy Mwalimu; naye ana historia yenye kushabihiana kwa kiasi fulani na Rais Samia, kwani alibahatika kuwahi kukalia kiti kwenye Bunge Maalum la Katiba kwa utumishi wenye mafanikio.

Huyo ni mhitimu wa sheria katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, pia akaongeza daraja ngazi ya shahada ya uzamili ya fani hiyo katika Chuo Kikuu cha Pretoria, Afrika Kusini na ametumika katika sehemu mbalimbali serikalini, pia mashirika yanayojihusisha kitaaluma katika uongozi, sheria, na utawala bora.

Amekuwa Mbunge wa Viti Maalum vya Wanawake katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 nafasi aliyotumikia na baadaye akagombea ubunge wa jimbo. Muda wote huo, ametumika katika baraza la mawaziri, akiwa mwenyeji zaidi kwenye Wizara ya Afya. Pia ameshawahi kuwa Mjumbe wa Halmshauri Kuu ya CCM.

Dk. Stergomena Lawrence Tax; Huyo ana upekee wake, akiweka historia kuwa mwanamke wa kwanza kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na kabla ya hapo kuteuliwa mwaka huu, alikuwa Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)

Awali kabla ya kuondoka nchini alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki tangu 2008 hadi 2013. Elimu yake, ana Shahada ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; pia shahada za uzamili na uzamivu katika siasa na uchumi wa maendeleo, amezipata kutoka Chuo Kikuu cha Tsukuba huko Japan alikohitimu mwaka 2002.

Dk. Ashatu Kijaji; ni Mbunge msomi anayewakilisha jimbo la Kondoa mkoani Dodoma, akitumikia katika nafasi ya Naibu Waziri, kuanzia mwaka huu ni Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

Elimu yake inaanzia katika Chuo cha Maendeleo ya Uongozi (IDM), Mzumbe akizamia katika eneo la mipango, na baada ya kuhitimu, alitumia wadhifa wa elimu yake, Ofisa Mipango wa Wilaya ya Kisarawe. Baadaye alijiendeleza kwa masomo ya uzamili chuoni Mzumbe ambako alifanya vizuri na kubakia chuoni kuwa mhadhiri na kisha alijiendeleza nchini Norway, mwaka 2013 alitunukiwa shahada ya uzamivu. Alijitosa kwenye siasa za ubunge tangu mwaka 2015 akiendelea kutumikia hadi sasa.

Dk. Dorothy Gwajima; Kitaaluma ni daktari wa tiba za binadamu, na amekuwa akitumikia fani yake kwa nyadhifa mbalimbali hadi kufikia ngazi ya juu kuwa Mtendaji Mkuu (Katibu Mkuu) wa Wizara ya Afya, kabla ya kuteuliwa kuwa mbunge na kupandishwa daraja kuwa mkuu wa wizara, Waziri wa Afya.

Hata hivyo, katika mabadiliko ya wizara hivi karibuni, sehemu ya iliyokuwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia ,Wazee na Watoto, kuundiwa wizara mpya, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Daktari Gwajima, anayesifika kuwa 'jembe' kwa majukumu yake, amehamishiwa huko kuwa waziri anayeiongoza.

Dk. Angeline Mabula; msomi huyo wa uhasibu kwa sasa ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Mkazi, na kabla ya hapo kwa miaka kadhaa ameshatumikia utumishi wa umma katika ngazi ya wilaya.

Ni mhitimu wa Taasisi ya Usimamizi wa Fedha (IFM), pia kajiendeleza kitaaluma katika taasisi nyingine za kielimu, ikiwamo Chuo Kikuu Huria (OUT), alikopata stadi ya Maendeleo ya Jamii na Uchumi.

Hivyo, katika hali ya kawaida, inaweza kurejesha nafsi ya mtu anayefanyia tathmini 'majembe' kinamama katika kikosi kazi cha juu cha Rais Samia Suluhu Hassan, hata akaling'arisha taifa kwa ufanisi ndani ya mwaka mmoja unaotimu wiki hii.

Kwa lugha ya kiungwana, huhitimishwa kwa kauli hongera kinamama!





## NHC yapatiwa mkopo nafuu wa bil. 20/-

Na Paul Mabeja, DODOMA

SERIKALI imelipatia Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) mkopo nafuu wa Sh. bilioni 20 zitakazotumika kama mtaji ili kuwezesha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa nyumba 1,000 za makazi jijini Dodoma.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Allan Kijazi, alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema mkopo huo ni wa miaka 15 ambao utalipwa kwa muda wa miaka 12 baada ya miaka mitatu ya kipindi cha ujenzi wa mradi wa nyumba 1,000.

"Azma ya serikali ni kuliwezesha Shirika la Nyumba la Taifa, kujenga nyumba hapa Dodoma ili kusaidia upatikanaji wa makazi na hasa baada ya uamuzi wa serikali kuhamishia shughuli zake jijini Dodoma," alisema.

Dk. Kijazi alisema fedha za mkopo huo riba yake ni nafuu ya asilimia 6.75 ambazo zimetolewa na serikali kupitia Benki ya Azania.

"Benki hii pia imekubali kuwakopesha wanunuzi wa nyumba za Iyumbu kwa riba nafuu sana ya asilimia tisa, awamu ya pili na ya tatu kwa kutumia fedha zinazopatikana baada ya kuuza nyumba ambazo zimeshakamilika," alisema.

"Awamu ya kwanza ya mradi wa nyumba 1,000 unaotekelezwa na Shirika hapa Dodoma ulianza Januari 6, mwaka 2021, kwa eneo la Iyumbu na Chamwino ulianza Februari 1,2021, mradi huu mkubwa unahusisha ujenzi wa nyumba za makazi 1,000 katika Jiji la Dodoma utagharimu Sh. bilioni 71 hadi kukamilika, awamu hiyo ya kwanza yenye nyumba 404," alisema.

Kadhalika, alisema awamu ya pili ya mradi huo itahusisha ujenzi wa nyumba 325 na majengo sita ya kutoa huduma, pamoja na shule na eneo la zabuni, awamu ya tatu itakamilisha ujenzi wa nyumba 275.

# Fursa za mafunzo kwa vijana zaongezeka

Na Paul Mabeja, DODOMA

SERIKALI imeendelea kutekeleza programu ya kukuza ujuzi nchini kwa kuongeza wigo wa fursa za mafunzo kwa vijana kutoka 10,113 kwa kipindi cha mwaka mmoja kilichoishia Machi, 2021 hadi 22,899 kwa kipindi cha mwaka mmoja kilichoishia Machi, 2022.

Aidha, wigo wa utoaji wa mafunzo umeongezeka kutoka vituo 17 katika mikoa 13 hadi vituo 72 mikoa 26.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, alibainisha hayo juzi wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema katika kipindi hicho serikali imewezesha mafunzo ya uzoefu wa kazi (Internship) kwa wahitimu 2,215 wa elimu ya juu na ya kati kupitia waajiri wa sekta binafsi na sekta ya umma.

"Kutoa mafunzo ya kurasimisha ujuzi walioupata nje ya mfumo rasmi kwa Watanzania 2,644 ambapo kati ya 2,537 wamefaulu na kupata vyeti vya VETA. Kuendelea na mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi kwa njia ya uanagenzi kwa vijana 14,440.

"Tumejenga vitalu nyumba (Greenhouse) katika halmashauri 36 za mikoa mitano ya Arusha, Dar es Salaam, Pwani, Tabora na Singida. Sambamba na ujenzi wa vitalu nyumba, vijana 720 wamepatiwa mafunzo ya ufundi wa kujenga vitalu nyumba," alisema.

Aidha, mafunzo ya namna ya kulima kwa kutumia vitalu nyumba yanaendelea kutolewa kwa vijana 3,600 (100 kutoka kila halmashauri).

"Idadi hiyo inafanya kuwa jumla ya vijana 12,850 kutoka halmashauri 117 na mikoa 17 ambao wamepatiwa mafunzo hayo," alisisitiza Prof. Ndalichako.

Vilevile, alisema katika kuhakikisha wanawezesha Watanzania kunufaika na fursa za ajira za ndani na nje ya nchi, serikali imewezesha wajasiriamali kushiriki katika maonyesho ya 21 ya wajasiriamali wadogo na wa kati wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyofanyika jijini Mwanza mwezi Desemba, 2021.

"Katika maonyesho hayo, jumla ya wajasiriamali 1,104 kutoka nchi sita za Jumuiya ya Afrika Mashariki walishiriki na kati yao Watanzania walikuwa 469," alisema.

Kadhalika alisema washiriki wa maonyesho hayo walipata fursa za kurasimisha shughuli, kutangaza bidhaa zao, kubadilishana taarifa, kukuza ujuzi na masoko ya bidhaa na huduma.

Alisema wajasiriamali wamepatiwa mafunzo na taasisi za ubora wa bidhaa na urasimishaji wa shughuli kama vile BRELA, TBS, TMDA, TRA, TANTRADE na NSSF.



Mafundi wa kampuni ya ujenzi ya Mohammed Builders Ltd, wakiendelea na ujenzi wa mradi wa soko la wafanyabiashara wadogo maarufu machinga, katika eneo la Bahi Road, jijini Dodoma jana. Eneo hilo, linatarajiwa kutumiwa na idadi ya wamachinga zaidi ya 4,000. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Zahanati yakabiliwa uhaba wa magodoro

Na Paul Mabeja, DODOMA

ZAHANATI ya Ihumwa jijini Dodoma inakabiliwa na uhaba wa magodoro pamoja na ufinyu wa chumba kwa ajili ya wajawazito kujifungulia hali inayosababisha wengi wao kuruhusiwa kabla ya muda unaotakiwa kitaalamu.

Mganga Mfawidhi wa zahanati hiyo, Aisha Abubakary, alibainisha hayo juzi wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kero mbalimbali zinazo ikabili zahanati hiyo.

Alisema hivi sasa chumba kinachotumika kwa ajili ya kinamama kujifungua ni kidogo ikilinganishwa na idadi ya wanaopatiwa huduma kila siku.

"Hivi sasa chumba hiki ni kidogo sana, lakini pia kina magodoro mawili tu na kinamama wanaojifungua kila siku ni wastani wa wanne hadi watano," alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo, wanalazimika kuwaruhusu kinamama waliojifungua kabla ya muda ili kupata nafasi ya wengine kupatiwa huduma.

"Kutokana na idadi ya wajawazito wanaojifungua kila siku na uhaba wa magodoro na ufinyu wa chumba inatulazimu kuwaruhusu wengine waliojifungua kurudi nyumbani kabla ya ule muda wa saa 24 hadi 48 unaoshauriwa kitaalamu," alisema.

Alisema wanaiomba serikali kuwasaidia ili kupata chumba kikubwa ambacho kitatumika na wajawazito kujifungua.

"Hili eneo lina watu 12,642 ambao wanaitegemea zahanati hii, lakini kila mwaka zaidi ya kinamama 427 wanapatiwa huduma ya kujifungua hapa," alisema.

Alisema kero nyingine ni kukosekana kwa chumba cha maabara hali inayowalazimu kubeba vipimo kila siku kupeleka katika hospitali nyingine kwa uchunguzi.

"Jengo la maabara lipo, lakini halijakamilika ni nguvu za wananchi ambazo walijitoa na kuanzisha ujenzi na lilitarajiwa kuanza kutumika mwaka jana, lakini hadi sasa bado halijakamilika," alisema.

Alisema kero nyingine ni ufinyu wa chumba, upimaji pamoja na kukosekana kwa uzio.

Ofisa Muuguzi wa zahanati hiyo, Tabitha Nyansika, alisema wanashukuru baadhi ya wadau wanaojitolea misaada ya magodoro kwa kuwa awali walikuwa na magodoro matatu, moja OPD na mawili wodi ya wazazi hali iliyokuwa ikisababisha wajawazito kupata wakati mgumu pale wanapojifungua.

"Walikuwa wanajifungua kwa kupokezana sasa unakuta wakati fulani inatokea wanakwenda kwa pamoja hivyo inabidi uwaruhusu kurudi nyumbani kabla, wengine kabla ya kufikisha muda ule wa kitaalamu wa saa 24 hadi 48 ili kutoa nafasi kwa wengine kujifungua," alisema Nyansika.





# BRELA yawanoa maofisa biashara 50

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imeanza kutoa mafunzo maalumu kwa maofisa biashara zaidi ya 50 kutoka mikoa ya Mbeya, Songwe na Rukwa ya utekelezaji wa sheria za leseni na biashara baada ya kubaini kuwapo matatizo ya utoaji wa leseni.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano kutoka BRELA, Roida Andusamile, alisema hayo wakati wa mafunzo yanayofanyika jijini hapa yanayolenga kuwajengea uwezo maofisa hao.

Andusamile alisema kumekuwapo na tatizo la utoaji wa leseni za biashara za daraja A na B kwenye halmashauri na leseni hizo hawapaswi kuzitoa kwa wafanyabiashara na badala yake zinatolewa na BRELA pekee.

"Tunatoa haya mafunzo kwa ajili ya kukumbushana utoaji wa leseni kwa maofisa biashara ili tuwe na lugha ya pamoja na tulialika maofisa biashara 80 kutoka mikoa ya Rukwa, Mbeya na Songwe, lakini wamefika 50 pekee, tunaamini hawa waliofika watafikisha ujumbe kwa wenzao," alisema Andusamile.

Awali, Ofisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Godfrey Nyaisa, alisema wakala huo uko kwenye utaratibu wa kuondokana na utoaji wa leseni za vitabu kwenye halmashauri na badala yake zitatolewa kwa njia ya mtandao. "Hizi leseni ambazo zinatolewa na halmashauri kwa maana ya vitabu ambavyo maofisa biashara wanaomba BRELA tunataka tuboreshe badala ya kutumia hata kopi sasa tutatumia mifumo," alisema Nyaisa.

Akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema serikali inahitaji maofisa biashara ambao wanaisaidia nchi kwa kuwa wabunifu na kuongeza uwajibikaji hasa katika suala la kuongeza uwekezaji.

Aliwataka maofisa biashara kuwa wabunifu kwa kufanya kazi ya kutafuta wawekezaji kwa ajili ya kuinua uchumi wa taifa ikiwa ni pamoja na kuwa wabunifu.

"Tutoke nje ya boksi, haipendezi kuwa na ofisa biashara anayekaa ofisini, tokeni nje nendeni mkaongee na wawekezaji, wafanyabiashara shaurianeni na kujadiliana nini kifanyike kuwa na uwekezaji kwenye maeneo yenu," alisema Homera.

Hata hivyo, baadhi ya maofisa biashara kutoka mikoa hiyo, walisema mafunzo hayo yamekuja muda muafaka na yameonyesha kundi hilo linathaminiwa na serikali.

Ofisa Biashara wa Mkoa wa Mbeya, Stanley Kibakaya, alisema mafunzo hayo yatawaongezea weledi katika kusimamia biashara kwenye maeneo yao pamoja na kuwa wabunifu.

Alisema maofisa biashara ndiyo injini ya biashara na uwekezaji katika maeneo ya mikoa yao na kuomba waendelee kupatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akizungumza wakati wa kufungua mafunzo maalumu kwa maofisa biashara kutoka mikoa mitatu ya Mbeya, Songwe na Rukwa, yaliyoandaliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), jijini Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Wazazi CCM kukodisha shule zake zilizoshindwa kujiendesha

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

JUMUIYA ya Wazazi ya Chama cha Mapinduzi (CCM), imesema inakusudia kuikodishia Serikali baadhi ya shule zake ambazo zimeshindwa kujiendesha kwa faida na zilizopoteza matumaini ya kuendelea.

Jumuiya hiyo imesema inakusudia kuanzisha shule za vipaji maalumu katika kila mkoa nchini ili kuongeza ubora wa elimu hasa kwenye shule zinazomilikiwa na jumuiya hiyo nchini.

Hayo yalisemwa juzi wilayani Mbarali katika Mkoa wa Mbeya na Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo Taifa, Dk. Edmund Mndolwa, alipokuwa anaweka jiwe la msingi kwenye mradi wa ujenzi wa nyumba ya Katibu wa Jumuiya ya wazazi ya wilaya hiyo.

Dk. Mndolwa alisema baadhi ya shule za jumuiya hiyo hazina mwenendo mzuri na ili ziwe na ufanisi inatakiwa kubadili mfumo wa uendeshaji.

Alisema kwa sasa baadhi ya shule hizo haziinufaishi jumuiya hiyo na zingine zinaendeshwa kwa hasara tofauti na makusudio ya kuanzishwa kwake.

"Tumefikia uamuzi huu ili shule hizi ziinufaishe Jumuiya yetu kiuchumi, hatuwezi kuendelea kuendesha taasisi hizi kwa hasara, tumeona ni vyema tuingie mkataba na serikali namna ya uendeshaji wa shule hizi kwa faida," alisema, Dk. Mndolwa.

Alisema Jumuiya hiyo ina miradi mingi inayoendeshwa kwa faida na haiwezi kuendelea kushughulika na shule hizo ambazo uendeshaji wake sio mzuri.

Hata hivyo, alisema Jumuiya hiyo inakusudia kufuatilia kwa kina ili kubaini chanzo cha kutofanya vizuri shule hizo kabla ya kuendelea na utaratibu wa kuzikodisha.

Kwa upande wake Katibu wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Mbeya, Amina Songoro, alisema shule hizo zinakabiliwa na matatizo mbalimbali ambayo yanasababisha uendeshaji wake kuwa mgumu na kuwa wa hasara.

Alisema jumuiya hiyo kwa sasa inadaiwa fedha nyingi na Mamlaka ya Ukusanyaji wa Mapato nchini (TRA) kutokana na kutolipa mapato kwa muda mrefu na hilo ni miongoni mwa matatizo yanayozikabili shule hizo.

Vilevile, alisema baadhi ya shule hizo miundombinu yake imechakaa na inahitaji fedha nyingi kufanyiwa marekebisho na kwamba baadhi ya shule wanafunzi wana nidhamu mbovu.

Awali, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakasole, alimuomba Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi kusaidia kwenye utatuzi wa mgogoro wa mipaka kati ya wananchi na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Alisema mgogoro wa mipaka hiyo unasababishwa na Tangazo la Serikali namba 28 la mwaka 2008 (GN.28) ambalo baadhi ya mipaka yake inaingia kwenye makazi ya watu pamoja na taasisi za umma.

Alisema mgogoro huo ambao ni wa muda mrefu umekuwa ukikisumbua chama hicho na kusababisha wananchi wa wilaya hiyo kuichukia serikali pamoja na chama hicho tawala na kwamba wananchi wanashindwa kufanya shughuli za maendeleo..

# Wanawake wadaiwa kushawishi watoto wasifanye vizuri shuleni

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

BAADHI ya wanawake katika Kijiji cha Ilasilo Kata ya Garula wilayani Songwe, wanadaiwa kuwa vinara wa kuwashawishi watoto wao wa kike kutofanya vizuri kwenye mitihani ili wawaozeshe na kujipatia mali jambo ambalo linahesabika kama ni ukatili wa kijinsia.

Diwani wa Viti Maalumu Kata ya Garula, Pascalina Shitundu, aliyasema hayo juzi wakati wa mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Shirika la Maendeleo la ADP Mbozi na kufanyika katika Kijiji cha Ilasilo.

Shirika la ADP Mbozi linahusika na mradi wa uhakika wa chakula katika familia na kusema wanawake hao wamekuwa wakikiuka haki za msingi za watoto kwa kuchochoea ndoa za ututoni na kata hiyo ni miongoni mwa maeneo ambayo mradi unatekelezwa.

Alisema tabia hiyo inamsikitisha kwa sababu wanawake wenzake ambao walitakiwa wawe wanapambana na ukatili dhidi ya watoto, wamegeuka kuwa vinara wa kushiriki vitendo hivyo.

"Ninasikitika kwamba wanawake wenzangu ndiyo mnawahamasisha watoto wasifanye vizuri kwenye mitihani ili muwaozeshe, sasa unamuozesha mtoto mdogo ili akafanye nini kwenye ndoa? Nawaombeni wanawake wenzangu tuwasaidie watoto wetu," alisema Pascalina.

Mwakilishi wa Shirika la ADP Mbozi, Jackline Sanga, alisema wanawake wamemukuwa wakikabiliana na matatizo mbalimbali yakiwamo ya ukatili pamoja na mabadiliko ya tabia nchi ambayo yanasumbua dunia kwa sasa.

Alisema watoto wa kike wanaanza kupata matatizo ya ukatili wa kijinsia kuanzia kwenye familia, shuleni na kwenye ndoa na kwamba kila mdau anatakiwa kushiriki kwenye ulinzi huo.

Aliwataka wananchi kuwasaidia watoto wa kike kwenye mambo mbalimbali ikiwamo kuwasaidia kupata nafasi za uongozi ili kuwa na usawa kwenye jamii.

Kaimu Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Songwe, Wambi Mwalukisi, alisema hivi karibuni halmashauri hiyo iliwaokoa watoto watatu ambao walikuwa wanasafirishwa kwenda kutumikishwa kwenye kazi za ndani.

Alisema baadhi ya watoto hao ni waliokuwa wamefaulu darasa la saba na kutakiwa kujiunga na kidato cha kwanza, lakini wazazi wao wakaamua kuwapeleka kwenye vibarua.

"Mmoja wa watoto hao alikuwa darasa la sita akaachishwa shule na wazazi wake na kuozeshwa kwa mtu mzima, sasa hivi vikundi vya makuzi na malezi vilisaidia kumuokoa," alisema Wambi.

Alisema vikundi vya makuzi na malezi vilivyoanzishwa kwenye jamii vinasaidia kutoa taarifa za ukatili dhidi ya watoto na wanawake kwenye jamii.



## HABARI ZANZIBAR

# Rais Mwinyi afurahia ujio Rais wa FINA

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema kuwa ujio wa Rais wa Shirikisho la mchezo wa kuogelea duniani (FINA), Zanzibar utasaidia kwa kiasi kikubwa kuitangaza Zanzibar kiutalii hasa katika utalii wa michezo.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana alipokutana na Rais wa FINA, Hussain Al Musallam, akiwa na ujumbe wake wa viongozi mbalimbali wa shirikisho hilo kutoka ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakiwamo waliotoka Makao makuu ya FINA nchini Switzerland.

Katika mazungumzo hayo Dk. Mwinyi alisema kuwa mchezo huo ni maarufu duniani na ujio wa kiongozi huyo utasaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha uhusiano na ushirikiano kati ya Zanzibar na FINA.

Kadhalika, alisema hatua hiyo itaisaidia Zanzibar ambayo imezungukwa na bahari, na iliyo katika mikakati ya kuimarisha Sera ya Uchumi wa Buluu, miongoni mwa malengo iliyojiwekea ni kuimarisha sekta ya utalii kwa kupitia utalii wa michezo.

"Tumefurahishwa kwa kiasi kikubwa na ujio wa Rais wa Shirikisho la mchezo wa kuogelea duniani (FINA) Hussain Al Musallam ambapo kuja kwake hapa Zanzibar kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha ushirikiano katika sekta ya michezo nchini," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema kuwa ujio wa kiongozi huyo ni mwanzo mzuri wa ushirikiano katika kukuza sekta ya michezo ikiwamo utalii wa michezo ambao kutokana na mazingira ya Zanzibar mafanikio makubwa yanaweza kupatikana. Rais Mwinyi alisema kuwa ziara ya kiongozi huyo ni nafasi nzuri kwa Zanzibar kwa kuwa itasaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha sekta ya michezo ambayo hivi sasa imewekewa mikakati maalum.

Alieleza haja kwa Zanzibar kuwa mwanachama wa FINA hatua ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kujifunza mambo kadhaa kutoka Shirikisho hilo ambalo limepata mafanikio makubwa.

Rais Mwinyi alimkaribisha Zanzibar Rais wa FINA na kumueleza mikakati na malengo yaliyowekwa na serikali anayoiongoza katika kuimarisha sekta ya michezo hapa nchini ukiwemo utalii wa michezo.

Naye Rais wa FINA, Al Musallam alimueleza Rais Mwinyi kwamba kuogelea si mchezo tu bali ni sehemu ya maisha na vijana walio wengi wamekuwa wakiufuatilia.

Alisema miongoni mwa sababu kubwa ya ziara yake ya Zanzibar ni pamoja na kumuunga mkono Rais Mwinyi katika mikakati yake ya kuimarisha uchumi kupitia Sera ya Uchumi wa Buluu ambao sekta ya utalii wa michezo imejikita ndani yake.

Alisema hatua mbalimbali zilizowekwa na Shirikisho hilo katika kuhakikisha inaweka programu mbalimbali za mafunzo ya kuogelea kwa ajili ya vijana wa Zanzibar ambao watafaidika na programu hiyo.

# Asilimia 30 ya watoto wana udumavu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ASILIMIA 30 ya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano wana tatizo la udumavu wa mwili na kiakili, licha ya Tanzania kuwa na uhakika wa chakula.

Hayo yalielezwa na Mwakilishi Msaidizi wa programu kutoka Shirika la Chakula na Kilimo (FAO) Charles Tulahi, wakati akizungumza na waandishi wa habari nje ya mafunzo ya kikanda ya warsha ya wakufunzi kuhusu zana mpya ya FAO na usimamizi bora wa dharura (GEMP), uliofadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) uliofanyika mjini hapa.

Alisema lazima kuwe na rasilimali watu yenye uwezo, kimwili na kiakili ili kufikia malengo ya maendeleo ya nchi.

"Tunahitaji kuwekeza katika uzalishaji wa rasilimali watu wenye uwezo, lakini kiwango cha asilimia 30 ya watoto waliodumaa nchini kinatia wasiwasi," alisema.

Alisema FAO inapanga kampeni kabambe kuhusu lishe ili kupambana na utapiamlo nchini, litashirikiana na washirika wengine katika kampeni hiyo, ambayo imepangwa kuzinduliwa hivi karibuni.

Akieleza kuhusu warsha hiyo, Mkuu wa programu ya FAO, alisema inalenga kutoa kanuni za msingi za maandalizi na mipango ya dharura, kushiriki uzoefu wa washiriki husika na kuwapa ujuzi wa vitendo unaozingatia kanuni za GEMP.

Naye Ofisa Mkuu wa Idara ya Huduma za Mifugo Zanzibar, Dk. Talib Saleh Suleiman, alisema kutokana na Zanzibar kuwa kisiwa, ipo hatarini kwa magonjwa ya mlipuko ya wanyama, ambayo lazima idhibitiwe kwa gharama yoyote.

Dk. Talib ambaye ni daktari wa mifugo, alisema ugonjwa wa kichaa cha mbwa ni miongoni mwa hatari kwa wanyama visiwani Zanzibar na juhudi mbalimbali zinafanyika kuudhibiti ugonjwa huo ikiwamo kutoa chanjo kwa wanyama akiwamo mbwa na paka ili kudhibiti maambukizi kwa binadamu.

"Kichaa cha mbwa ni ugonjwa hatari sana kwa sababu unaambukiza wanadamu... na ndiyo maana tunatoa chanjo ya kichaa cha mbwa kila mwaka," alisema.

Alisema, homa ya Nguruwe na Bonde la Ufa ni magonjwa ya wanyama ambayo bado hayajapatikana Zanzibar, chini ya mfumo mmoja wa afya, madaktari wa mifugo wanashirikiana kukabiliana na changamoto ya maradhi hayo.

Mafunzo hayo ya siku nne yamewashirikisha washiriki kutoka Tanzania, Kenya, Uganda na Ethiopia, huku kila nchi ikiwa na washiriki watano.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Abdallah Hussein Mussa, akionyesha kwa waandishi wa habari, ofisini kwake jana, namba za gari za nje ya nchi pamoja na nyaraka mbalimbali alizokamatwa nazo Mtuhumiwa Yunus Nassor Ali. **PICHA: RAHMA SULEIMAN.**

# Wadau waombwa maoni uboreshaji hifadhi bahari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WADAU mbalimbali wametakiwa kutoa maoni yao kuboresha mpango mkuu wa serikali ili kukamilika na kuanza kutumika katika uendeshaji wa maeneo ya hifadhi za bahari na rasilimali zake.

Mkurugenzi wa Idara ya Uhifadhi wa maeneo ya Baharini Zanzibar, Dk. Makame Omar Makame, kutoka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, aliyasema hayo katika kikao cha kujadili rasimu ya GMP ya mipango mikuu ya uendeshaji wa maeneo ya hifadhi ya bahari, Maruhubi Mjini Unguja.

Dk. Makame alisema idara kupitia mradi wa swofishi imetafuta wataalamu wa kutengeneza mpango huo katika maeneo ya hifadhi ya bahari ya Tumca, Mimca, Chabamca na Ghuba ya Minai kwa lengo la kuona maslahi yanapatikana kwa kizazi cha sasa na baadaye.

"Tungekuwa hatukuyahifadhi maeneo tukaacha kila mtu afanye anavyotaka kungekuwa hakuna matumizi endelevu katika rasilimali za bahari," alisema Dk. Makame.

Alisema kutokana na wananchi wengi kutegemea bahari jambo ambalo husababisha uchafuzi wa mazingira, serikali imetenga maeneo makuu matano ya hifadhi za bahari kisheria mwaka 2014, manne Unguja na moja Pemba ili kuiweka bahari katika hali ya usalama.

"Miongoni mwa hifadhi hizo, Tumca na Chabamca ni mpya katika usimamizi wa kazi kwa mwaka fedha 2021 ambazo kwa upande wa Tumca imeanzia Kendwa, kisiwa cha Tumbatu hadi Nyanjale na Chabamca imeanzia Sharifu Msa na visiwa vidogo vya Bawe, Changuu hadi Mazizini," alisema. Dk. Makame alisema uhifadhi wa maeneo ya bahari unaleta faida kubwa katika kuimarisha rasilimali za bahari na kuongeza watalii.

Aidha, alisema serikali imepiga marufuku baadhi ya dhana za uvuvi za kuvulia katika maeneo ya hifadhi za bahari ili kuepusha uharibifu wa kimazingira usifanyike na kuzifanya shughuli za uvuvi kuwa endelevu.

Naye Meneja Mkuu wa Mpango wa Hifadhi za Bahari, Dk. Christopher Muhando kutoka Chuo cha Sayansi ya bahari alipendekeza kuwekwa utaratibu wa miundombinu katika maeneo ya utalii ili kuitangaza Zanzibar na kuifanya kuwa na vivutio mbalimbali.

Dk. Muhando aliziomba taasisi husika kuenda sambamba na shughuli wavuvi katika kufanya utafiti wa matumizi ya taa na umwagaji wa maji ndani ya bahari yanayochemshiwa dagaa ili kuona athari na faida zinazojitokeza kwa kushirikiana na wanajamii.

Kwa upande wake, Dk. Flower Msuya, Mtafiti wa mwani, aliitaka jamii kuyasimamia mapendekezo waliyoyapendekezwa kutokana kuwa watumiaji wakuu katika shughuli za uvuvi pamoja na kutumia rasilimali za bahari kwa mpangilio mzuri ili kuwa endelevu kwa kizazi cha sasa na baadaye.

Dk. Flower alisema lengo la kutumia mpango huo ni kutunza mazingira katika maeneo ya hifadhi ili kuzifanya hifadhi za bahari kuwa nzuri kwa sasa na miaka ya baadaye.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAPANGISHWA

**MAHALI:** KIHARAKA MAPINGA KARIBU NA KANISA LA TAG NI NYUMBA MPYA YA VYUMBA 3, SEBULE, JIKO NA PUBLIC TOILET KWA MAWASILIANO PIBA SIMU: **0655-529509 / 0711-622282 / 0714-421555**

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**PATRICK PETRO MLOWEZI anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaj aina ya TVS BAJAJI i yenye namba za usajili MC 904 AYP,chasisi namba 133637,engine namba 0K4KD1023543,yeyote atakayeiokotab atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa DAR/GOG/RB/424335/2021**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **WAITARA ERADIUS METHODI** wa BUKOBA anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari aina ya STARLET lenye namba za usajili **T823CAK.** Kadi hiyo yenye majina ya HASSAN ISSA wa S.L.P 533 Dar Es Salaam, ina Tin namba **102572823.**
Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/61545/2022.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi au apige simu namba **0763344049.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**RAHEL NSEMWA NKOMELA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI MC. 679 CQJ.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TARIFA YA POLISI MBE/CHU/RB/104360/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GRACE JAPHETH MILLINGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 151** AMT aina ya DATSUN, Chassis No. C**GD21005846,** Engine **No.216069514.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi, Taarifa ya Polisi **DOD/DOD/RB/98436/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO**
**Unapojibu tafadhali taja:**
**Kumb.Na: MMC/LD/18921**
**Tarehe: 09.03.2022**
**JOSEPH DAVIES NGODA,**
**S.L.P 643, MOROGORO.**
**YAH: NIA YA KUTOHUISHA MILIKI YA KIWANJA NA. 301 KITALU"-" KILAKALA**

**Rejea kichwa cha habari hapo juu.**
Kiwanja Na.301 Kitalu-Kilakala hapo awali kilitolewa kwa ndugu Joseph Davies Ngoda kupitia Hati Na. 28039 iliyotolewa muda wa miaka 33 kuanzia tarehe 1/10/1981 kwa matumizi ya makazi miliki hiyo ilikwisha muda wake tangu tarehe 30/09/2014.Aidha mwaka 1999 ilitolewa pia Barua toleo (Ofa) kwa Ndugu Zuberi M.Shabani ambaye ndiye anaishi kwenye makazi hayo hadi sasa kwa miaka 23 amekuwa akiishi hapo na ameendeleza kwa kujenga nyumba ya makazi.
Kupitia fungu la 32 la sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 Ofisi haina nia ya kuendelea kuhuisha milki ya Ndg Joseph Davies Ngoda kwani alishindwa kuendeleza kiwanja hicho kwa kufuata kanuni na taratibu.
Aidha tunakusudia kumilikisha milki hii kwa Ndg Zuberi M.Shaban ambaye ameendeleza kiwanja hicho na ndio anakaa hapo kwa miaka 23 tangu apewe barua ya toleo
Hivyo mtu yeyote mwenye pingamizi au maslahi juu ya kiwanja hiki anatakiwa kutoa taarifa kwa Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Morogoro S.L.P 587 Morogoro ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya barua hii.

VALENCY H.K
K.N.Y MKURUGENZI WA MANISPAA
MOROGORO

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**SONGELA ERNEST LYANGA** Mjini Masumbwe,anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC. 882 BEJ** aina ya **SANLG.**
Yoyote atayeiona atoae taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.
Taarifa ya polisi **GEI /MBO/ RB/ 38985/ 2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **GURVINDER SINGH KARWAL** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **ISUZU PICKUP DOUBLE CABIN** yenye namba za usajili T 247 ANF. Engine **NO: 833826.** Kwa yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha Polisi: **TAN/RB/106671/2022.**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

SIKU 21 MASHAMBULIZI RUSSIA-UKRAINE



Wanajeshi wanawake wa kujitolea wakiwa kwenye mafunzo mjini Kyiv. **PICHA: MTANDAO**

# NATO yazuru Ukraine, idadi ya wakimbizi sasa milioni 3

**Kyiv,** UKRAINE

MAWAZIRI wakuu watatu kutoka nchi tatu Ulaya, zilizoko kwenye Jumuiya ya Kujihami (NATO) wanapanga kufanya ziara katika mji mkuu wa Ukraine, Kiyv.

Viongozi wa Poland, Jamhuri ya Czech na Slovakia wanaenda kwenye mji huo kuonyesha mshikamano na Ukraine wakati licha ya majeshi ya Russia kuzidi kuusogelea mji mkuu huo na kuwa eneo hatari.

Waziri Mkuu wa Poland, Mateusz Morawiecki, Janez Jansa wa Slovakia wataungana na Petr Fiala wa Jamhuri ya Czech, wanakwenda Kyiv kama ujumbe wa Umoja wa Ulaya (EU), kukutana na Rais wa Ukraine, Volodymir Zelensky.

Serikali ya Poland imesema ziara hiyo ya maofisa wa ngazi ya juu imeratibiwa na Rais wa Baraza la Umoja wa Ulaya, Charles Michel na Rais wa Halmashauri Kuu ya Umoja wa Ulaya, Ursula von der Leyen.

### ZELENSKY ATOA WITO EU

"Ulaya lazima ilinde usalama kwa kuisaidia Ukraine dhidi ya Russia," Rais Zelenskiy amesema hayo akizungumza kwenye mkutano wa wakuu wa jeshi uliofanyika jana jijini London kwa njia ya video huku akisisitiza wampatie silaha zaidi.

"Mjisaidie wenyewe kwa kutusaidia sisi."

Rais huyo amesema kwamba pamoja na Russia kuwekwa vikwazo kadhaa vya kiuchumi, anadai bado havijatosha.

### UMOJA WA MATAIFA

Ikiwa ni siku ya 21 tangu Russia ilipoishambulia Ukraine, idadi ya wakimbizi imefika takribani milioni tatu huku nusu yao wakielekea Poland.

**Wakati vikosi vyetu vinaendelea na mashambulizi, vimeliteka pia eneo la makazi la Stepne. Kundi la wanajeshi wa Jamhuri ya watu wa Luhansk linaendesha operesheni katika Wilaya za Kaskazini Mashariki mwa mji wa Severodonetsk.**

Msemaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Wakimbizi, Paul Dillon, amewaambia waandishi wa habari mjini Geneva, Uswisi, jana.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, amehimiza hatua za kusitisha mapigano na kutafuta amani.

Hata hivyo wajumbe wa Russia na Ukraine walipanga kufanya awamu nyingine ya mazungumzo jana

pande hizo mbili zilielezea matumaini kuwapo kidogo hapo awali.

### NGANO BEI JUU AFRIKA

Katibu Mkuu UN, Guterres, ameonya kwamba vita vya Russia dhidi ya Ukraine vinaweza kusababisha kile alichokiita kimbunga cha njaa na uhaba wa chakula kote duniani.

Amesema nchi nyingi za Afrika na maskini zinategemea zaidi uzalishaji wa ngano wa Russia na Ukraine, ambayo sasa iko hatarini kutokana na mzozo huo.

Nchi hizo ni pamoja na Burkina Faso, Somalia na Yemen ambazo tayari zinahangaika kulisha watu wao.

Guterres ametoa wito wa kusitishwa kwa vita hivyo mara moja ili kuepuka kuharibika kwa mifumo ya chakula duniani.

Pia ametangaza kifurushi kingine cha Dola milioni 40 kusaidia mamilioni ya Waukraine wanaokabiliwa na njaa na kupungua kwa usambazaji wa maji na dawa.

### PETROLI BEI JUU

Afrika Mashariki nchini Kenya, Wakenya kuanzia jana, walianza kulipia zaidi mafuta huku uvamizi wa Russia dhidi ya Ukraine ukiendelea kuathiri bei ya mafuta ghafi na bidhaa zake.

Mamlaka ya Kudhibiti Mafuta Kenya, imesema bei ya petroli na dizeli itaongezeka kwa shilingi tano za Kenya sawa na Dola 0.044.

Mamlaka hiyo, imesema bei ya mafuta ya taa, ambayo hutumiwa na watu wengi wa kipato cha chini Kenya kupika, haitabadilishwa.

Mpango wa ruzuku ya mafuta ya petroli nchini Kenya umedumisha bei ya mafuta kwa miezi minne mfululizo.

Baada ya Russia kuvamia Ukraine, mafuta ghafi ya Brent yaliongezeka mara dufu katika kipindi cha miaka 14. Bei ya bidhaa muhimu pia inatarajiwa kuongezeka nchini humo.

### MASHAMBULIZI YAENDELEA

Vikosi vya Russia vimezidisha mashambulizi yake kwenye mji mkuu wa Ukraine, Kyiv, wakati wapatanishi wanakutana tena katika duru nyingine ya mazungumzo ya kusitisha mapigano.

Mashambulizi hayo yaliyofanyika mapema jana Jumanne asubuhi kwenye maeneo ya makazi ya watu mjini humo, yanadaiwa kuua takribani watu wawili.

Jengo la ghorofa 16 katika Wilaya ya Sviatoshynsky na jingine lenye ghorofa 10 kwenye eneo la Podilsk yameshambuliwa katika mashambulizi hayo ya anga.

Maofisa wa huduma za dharura wamesema kuwa zaidi ya watu 27 wameokolewa katika mashambulizi hayo. Pia Russia inaeleza kuudhibiti mkoa wa Kherson.

Jeshi la Urusi limesema limechukua udhibiti kamili wa Mkoa wa Kherson, Kusini mwa Ukraine.

Eneo hilo lililoko katika Bahari Nyeusi ni makazi ya watu wapatao milioni moja.

Msemaji wa Wizara ya Ulinzi ya Urusi, Igor Konashenkov amesema pia majeshi ya Russia yamedhibiti maeneo mingine.

"Vikosi vya wanajeshi vya shirikisho la Russia, vimechukua udhibiti kamili wa eneo lote la Mkoa wa Kherson.

"Wakati vikosi vyetu vinaendelea na mashambulizi, vimeliteka pia eneo la makazi la Stepne. Kundi la wanajeshi wa Jamhuri ya watu wa Luhansk linaendesha operesheni katika Wilaya za Kaskazini Mashariki mwa mji wa Severodonetsk," amefafanua Konashenkov.

Katika taarifa yake fupi ya kila siku aliyoitoa Jumanne, Konashenkov amesema mali kadhaa za jeshi la Ukraine zimeharibiwa, ikiwamo ndege za kivita, helikopta na makombora 13.

Ukraine imesema inataka amani, usitishaji wa mapigano mara moja na kuondolewa kwa wanajeshi wa Russia. Rais Zelensky amesema mazungumzo ya juzi yalikuwa mazuri.

Mshauri Mkuu wa Utumishi katika Ikulu ya Ukraine, Oleksiy Arestovich amesema makubaliano ya amani yanaweza kufikiwa ifikapo mwezi Mei.

Amesema huenda vita kati ya Russia na Ukraine vikamalizika ifikapo mwezi Mei mwaka huu au pengine mapema zaidi, kulingana na maendeleo ya sasa.

**Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao**

# POULSEN AMUITA TEPSI STARS, NYONI, MSUVA WAACHWA

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa timu ya Taifa ya Tanzania, (Taifa Stars), Kim Poulsen amemjumuisha kwa mara ya kwanza katika kikosi hicho, winga kinda wa Azam FC, Tepsi Evance, katika kikosi chake kitakachoingia kambini kujiwinda na mechi mbili za kirafiki za kimataifa dhidi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati na Sudan.

Aidha, katika kikosi hicho cha wachezaji 24 kitakachoingia kambini Jumapili wiki hii, Poulsen amemwacha Erasto Nyoni wa Simba na Simon Msuvu (Wydad Casablaca- Morocco), lakini pia John Bocco ambaye ni majeruhi.

Stars inatarajiwa kuikaribisha katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jamhuri ya Afrika ya Kati Machi 23, kabla ya kushuka tena dimbani hapo Machi 28, mwaka huu kuvaana na Sudan, michezo hiyo ikiwa katika Kalenda ya Fifa.

Mbali na Tepsi, wachezaji wengine walioitwa katika kikosi hicho cha Poulsen ni Aishi Manula (Simba), Metacha Mnata (Polisi Tanzania), Shomari Kapombe (Simba), Israel Mwendwa (Simba), Lusajo Mwaikenda (Azam), Abdul Razack Hamza (Namungo), Muhamed Husein (Simba), Nickson Kibabage (KMC), Farid Musa (Yanga) na Novatus Dismas (Beitar Tel Aviv Bat Yam - Israel).

Wengine ni Mzamiru Yassin (Simba), Jonas Mkude (Simba), Zawadi Mauya (Yanga), Aziz Andawile (Mbeya City), Kelvin John (Genk - Ubelgiji), Feisal Salum (Yanga), Mbwana Samatta (Royal Antwerp - Ubelgiji), Reliant Lusajo (Namungo), Kibu Denis (Simba), George Mpole (Geita Gold) na Ibrahim Joshua (Tusker - Kenya).

Akizungumza na waandishi wa habari jana kwenye Ofisi za Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Poulsen alisema ameita sura mpya kutokana na kuridhishwa na uwezo wao, huku akisisitiza kutochukua wachezaji kutokana na ukubwa wa majina yao kwani anachokiangalia ni uwezo na si vinginevyo.

"Najua watu watashangaa kwa nini nimeita sura mpya kwenye kikosi ambacho kitaingia kambini wikiendi hii, ni kwa sababu wameonyesha uwezo mkubwa kwenye klabu zao wanazozichezea wakaniridhisha," alisema Poulsen.

Alisema kwa upande wake, michezo hiyo anaichukulia kwa umuhimu mkubwa kwani itamsaidia kupata wachezaji wazuri watakaounda timu ya taifa.

Alisema ameamua kuweka wachezaji chipukizi kwa kuamini watafanya vizuri katika timu ya taifa na kudai anemuingiza kwa mara nyingine Kelvin John kutona na ubora aliokuwa nao.

Alisema watakuwa na mashindano ya CHAN Julai, hivyo wanatakiwa kuhakikisha timu ya taifa inafanya maandalizi ya kutosha kuelekea michuano hiyo.

Aidha, alisema hajamuita Msuva kwa sababu mpaka sasa hajapata timu ya kuichezea baada ya kuwapo kwa mvutano na klabu yake ya Wydad Casablanca, na kwamba endapo atapata timu atamjumuisha ndani ya kikosi chake.

## Mtibwa Sugar yaivutia pumzi Kagera Sugar

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kuvuna pointi tatu katika mchezo wa Ligi Kuu mwishoni mwa wiki dhidi ya Geita Gold, Benchi la Ufundi la Klabu ya Mtibwa Sugar, limewapa mapumziko mafupi wachezaji wao ili kuiweka sawa miili yao kabla ya kurejea kambini kuwawinda ndugu zao, Kagera Sugar.

Jumapili iliyopita, Mtibwa Sugar ikiwa katika Uwanja wake wa Manungu Complex, Turian mkoani Morogoro, iliondoka na pointi tatu baada ya kuichapa Geita Gold mabao 2-0.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Salum Mayanga, alisema amewapumzisha nyota wake hao mpaka Ijumaa ya wiki hii watakaporejea kuanza maandalizi ya mechi ijayo dhidi ya Kagera Sugar itakayopigwa uwanjani hapo Aprili 3, mwaka huu.

"Baada ya kumaliza mchezo wetu na Geita Gold, niliwapa mapumziko wachezaji mpaka Ijumaa kila mmoja awe ameripoti kambini tayari kwa maandalizi ya mechi ijayo," alisema Mayanga.

Alisema kwa sasa amepata matumaini kwani ameona kikosi chake kikiendelea kuimarika katika mzunguko huu wa lala salama wa Ligi Kuu, tofauti na kilivyokuwa nyuma.

"Timu yangu inanipa matumaini, tumefanikiwa kupata pointi saba kwenye uwanja wetu wa nyumbani, si jambo dogo tumepata mwanga mzuri sasa," alisema.

Kuhusu mchezo ujao, alisema anafahamu Kagera ni timu nzuri, hivyo pamoja na maandalizi makubwa watakayofanya wataingia uwanjani kwa tahadhari kubwa wakiwa na lengo la kushinda kwa mara nyingine wakati huu wakicheza nyumbani.

Katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyopigwa Oktoba 22, mwaka jana kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, Mtibwa Sugar ambayo kwa sasa ipo nafasi 13 ikiwa na pointi 19 baada ya michezo 18, iliibuka na ushindi wa bao 1-0.

## KIPINDI KIPYA...



Mtayarishaji wa Kipindi cha 'Ya Walimwengu', Geah Habib, akizungumza na waandishi wa habari wakati wa hafla ya uzinduzi wa kipindi hicho kipya ndani ya DStv. Kipindi hicho kitakuwa kikiruka hewani kila Jumatano 3:30 usiku kupitia Chaneli 144 ya Maisha Magic Poa, inayopatikana katika kifurushi cha DStv Poa kwa Sh. 9,900 tu. **MPIGAPICHA WETU**

# KMKM, Mafunzo vitani robo fainali FA Cup leo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

ROBO fainali ya kwanza ya michuano ya Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF) maarufu FA Cup, itapigwa leo, ikiwakutanisha Mabaharia wa KMKM dhidi ya bingwa mtetezi wa kombe hilo, timu ya Mafunzo.

Mchezo huo unatarajiwa kupigwa katika Uwanja wa Amaan majira ya saa 1:15 usiku.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Mafunzo, Abdallah Bakari, alisema wamejipanga kusonga mbele katika michuano hiyo ili kutimiza lengo lao kubwa la kutetea ubingwa wao.

Alisema mchezo huo hautokuwa rahisi kutokana na ubora wa timu wanayokutana nayo, lakini lolote linaweza kutokea endapo wachezaji watacheza kwa lengo lilokusudiwa.

Alisema kuelekea mchezo huo wamewasihi wachezaji kucheza kwa umakini mkubwa na kwa tahadhari hasa kwa kuzingatia kuwa wanacheza na timu kubwa yenye uzoefu wa michuano ya kimataifa.

"Tumejipanga kufika hatua ya fainali na matumaini yangu ni kuwa lengo hili litatimia, tunakwenda kutetea ubingwa wetu na wachezaji wamehamasika kwa kiasi kikubwa, hivyo sina wasiwasi wa kupoteza," alisema.

Naye Kocha wa KMKM, Ame Msimu, alisema licha ya kuendeleza ndoto za kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu, lakini na Kombe la FA ni moja ya mipango yao kwa msimu huu.

"Mipango yetu ni kuupata ubingwa wa FA Cup na Ligi Kuu, hivyo mchezo huu wa hatua ya robo fainali ndio tunaanza safari katika michuano ya FA huku tukiendelea na mchuano mkali katika michezo ya ligi, nina matumaini makubwa kwa msimu huu malengo yetu kutimia," alisema.

Robo fainali ya pili itapigwa Machi 23, kati ya New King na Taifa Jang'ombe, huku ya tatu ikitarajiwa kupigwa Machi 25, kwa kuzikutanisha Zimamoto dhidi ya Umoja wa Mbuzini wakati robo fainali ya nne pakiwa na shuguli nyingine pevu kati ya KVZ na Kipanga Machi 31, mwaka huu na michezo yote itachezwa majira ya saa moja usiku katika Uwanja wa Amaan.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GERRARD AMWANIA SUAREZ

KOCHA wa Aston Villa, Steven Gerrard anamfuatilia mshambuliaji wa Atletico Madrid, Luis Suarez mwenye umri wa miaka 35, akiangalia uwezekano wa kumsajili nyota huyo wa Kimataifa wa Uruguay. (***Athletic***)

### UNITED KUMRUDIA KANE

MANCHESTER United itapeleka ofa mpya msimu wa majira ya joto kwa ajili ya mshambuliaji wa England na Tottenham, Harry Kane mwenye umri wa miaka 28. (***Mirror***)

### LUKAKU ATAJWA BARCA

BARCELONA itamgeukia mshambuliaji wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 28, kama watashindwa kumsajili straika wa Borussia Dortmund, Erling Haaland msimu huu. (***AS - via Star***)

### XAVI AMTAKA SALAH

KOCHA wa Barcelona, Xavi pia anataka kumwongeza kwenye kikosi chake mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 29. (***AS***)

### TISA KUMRITHI POCHETTINO

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta na wa Tottenham Antonio Conte wako kwenye orodha ya makocha tisa wa kuziba pengo la kocha wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino kama atafukuzwa. (***L'Equipe, via Mail***)

### BOTMAN ANUKIA MILAN

AC Milan inaamini itawasajili nyota wa Lille, mlinzi Sven Botman mwenye umri wa miaka 22 na kiungo, Renato Sanches, 24. (***90 Min***)

### KELLEHER HAUZWI - LIVERPOOL

GOLIKIPA wa Liverpool, Caoimhin Kelleher mwenye umri wa miaka 23, hatouzwa au kutolewa kwa mkopo katika dirisha lijalo la usajili, licha ya kusakwa na klabu nyingine za Ligi Kuu. (***Sun***)

### VIGOGO KWA LEWANDOWSKI

KLABU ya Manchester City inatarajiwa kungana na Real Madrid na Manchester United katika mbio za kusaka saini ya mshambuliaji wa Bayern Munich, Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 33, kama atakuwa sokoni mwishoni mwa msimu. (***Fichajes***)

### WORRALL NA WEST HAM

WEST Ham inaongoza juhudi zao za kumnasa mlinzi wa Nottingham Forest, Joe Worrall mwenye umri wa miaka 23, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Brentford na Everton. (***Sun***)

### RAPHINHA ATEGWA LEEDS

MSHAMBULIAJI wa Leeds United, Raphinha mwenye umri 25, anazivutia klabu ya Barcelona na Manchester United. (***Sportitalia***)

### DI MARIA ATAKIWA BENFICA

KLABU ya Benfica inamtaka mshambuliaji wa Paris St-Germain na Argentina, Angel di Maria mwenye umri 34. (***Record***).

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# XAVI: AUBAMEYANG NI ZAWADI KUTOKA PEPONI

●●● Yeye ni mchezaji mzuri ambaye mara zote huingia kwenye chumba akiwa katika hali nzuri na huzoea...

**BARCELONA,** HISPANIA

KOCHA wa Barcelona, Xavi amesema kwamba, mshambuliaji Pierre-Emerick Aubameyang ni kama zawadi kutoka peponi baada ya mchezaji huyo kufanya vizuri ndani ya Barcelona.

Aubameyang alifunga bao katika ushindi wa 4-0 dhidi ya Osasuna Jumapili akiwa amefunga mabao sita katika michezo tisa aliyocheza tangu atue Camp Nou akitokea Arsenal wakati wa dirisha la usajili la Januari.

**Auba ana wastani wa kufunga bao 0.96 ndani ya dakika 90 kwenye mashindano yote ukilinganisha na alivyokuwa kwa 'Washikabunduki' London, ambapo wastani wake uliKuwa ni 0.57 kwenye mashindano yote kabla ya kutimkia Barca.**

"Aubameyang ni zawadi kutoka peponi," Xavi alisema baada ya timu yake kupata ushindi wa nne mfululizo kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

"Yeye ni mchezaji mzuri ambaye mara zote huingia kwenye chumba akiwa katika hali nzuri na huzoea haraka mazingira mapya."

Barca wameingia katika wiki ya El Classico wakiwa katika kiwango bora kutokana na kutopoteza katika michezo 11 iliyopita kwenye mashindano yote.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,042

MECHI KALI
ARSENAL
VERSUS
LIVERPOOL
1 | 3.77
X | 3.82
2 | 1.88

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CHIELLINI KUMUIGA IBRAHIMOVIC



**TURIN,** Italia

GIORGIO Chiellini amedai kwamba, Zlatan Ibrahimovic ambaye ana umri wa miaka 40, amemhamasisha kwa kiasi fulani kuendelea kucheza mpira licha ya kufikisha umri wa miaka 37.

Akizungumzia uhusiano wake na Ibrahimovic, Chiellini alitania kwamba wanajadili kuhusu kustaafu kwao.

"Ndiyo, kama Ibra ataendelea na mimi pia nitaendelea, labda nimpigie simu na tunaweza kuamua," alisema katika mahojiano na The Times alipoulizwa kama maisha ya kucheza soka kwa muda mrefu ya Msweden huyo yamechangia mawazo yake kuhusu hatima yake.

"Kutoka zamani Ibra alikuwa ni adui yangu mkubwa," Chiellini aliongeza.

"Ibra anabahati mbaya kucheza katika zama za kina Lionel Messi na Cristiano Ronaldo sababu bila wao pengine angepata Ballon d'Or kadhaa.

## *EPL kurudisha 'sub' 5 msimu ujao*

**LONDON,** England

KLABU za Ligi Kuu England zinapanga kupiga kura ya kuamua matumizi ya mabadiliko ya wachezaji watano badala ya mfumo wa sasa wa mabadiliko ya wachezaji watatu, kwa mujibu wa BBC Sport.

Miongoni mwa ligi kubwa barani Ulaya, Ligi Kuu England ndio pekee inaendelea na mfumo wa 'sub' tatu badala ya tano ambazo zinatumika sehemu zingine.

Hii ni baada ya baadhi ya makocha na wachezaji kupaza sauti zao zikitaka mabadiliko hayo.

Ingawa kuna upinzani wa matumizi ya wachezaji watano (hasa kutoka katika klabu zenye wachezaji wachache), shirikisho la wachezaji wa kulipwa nchini Uingereza linaunga mkono mabadiliko hayo wakiamini kuwa, lengo kubwa ni kuwalinda wachezaji na si kuzibeba klabu kwa namna yoyote.

Juni 2022 inatajwa kuwa ndio mwezi wa maamuzi wakati ambapo, klabu zote za EPL zitakutana kwenye mkutano wa mwaka.

Pamoja na mabadiliko ya 'sub', pia kuna suala la muda kati ya mchezo mmoja na mwingine.

# 2,431,860

## JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/03/22 | 18:00 | Huddersfield vs Bournemouth | 2.51 | 3.29 | 2.65 |
| 02. 19/03/22 | 18:00 | Reading vs Blackburn | 2.60 | 3.25 | 2.75 |
| 03. 19/03/22 | 18:15 | Eupen vs Mechelen | 2.76 | 3.40 | 2.39 |
| 04. 19/03/22 | 20:45 | GO Ahead Eagles vs Cambuur | 2.48 | 3.45 | 2.70 |
| 05. 19/03/22 | 23:00 | Nantes vs Lille | 2.87 | 2.97 | 2.63 |
| 06. 20/03/22 | 14:30 | Venezia vs Sampdoria | 2.55 | 3.35 | 2.70 |
| 07. 20/03/22 | 15:30 | Jahn Regensburg vs Paderborn | 2.75 | 3.24 | 2.45 |
| 08. 20/03/22 | 16:00 | Gaziantep BB vs Galatasaray | 2.71 | 3.36 | 2.45 |
| 09. 20/03/22 | 17:00 | Bordeaux vs Montpellier | 2.40 | 3.45 | 2.80 |
| 10. 20/03/22 | 17:00 | Empoli vs Verona | 3.20 | 3.40 | 2.20 |
| 11. 20/03/22 | 18:00 | Ponferradina vs Eibar | 2.50 | 3.09 | 2.80 |
| 12. 20/03/22 | 18:15 | Celta Vigo vs Betis | 2.41 | 3.34 | 2.89 |
| 13. 20/03/22 | 20:00 | Roma vs Lazio | 2.34 | 3.41 | 2.96 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATANO - 16/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 2541 | Anyang vs Busan I Park | 2.09 | 3.17 | 3.27 |
| 14:00 | 2679 | Mohammedan SC vs Churchill Brothers | 1.94 | 3.37 | 3.46 |
| 14:00 | 5572 | Vipers SC vs Busoga United | 1.18 | 5.96 | 11.54 |
| 14:15 | 4225 | Shahrdari Astara vs Shahin Bushehr | 1.36 | 3.86 | 9.46 |
| 16:00 | 1900 | El Gouna vs Arab Contractors | 2.91 | 3.00 | 2.51 |
| 16:00 | 2009 | MSK Zilina vs Spartak Trnava | 2.51 | 3.29 | 2.51 |
| 16:00 | 2258 | Apollon 1926 vs Anagennisi Karditsas | 8.66 | 4.04 | 1.36 |
| 16:00 | 2447 | Paris St. Germain U19 vs FC Salzburg Youth | 1.83 | 3.77 | 3.48 |
| 16:00 | 2870 | Lusaka Dynamos vs Zanaco | 2.80 | 2.75 | 2.90 |
| 16:00 | 3532 | SC Villa vs Gaddafi FC | 2.55 | 3.15 | 2.85 |
| 16:00 | 4182 | Onduparaka FC vs Mbarara FC | 2.62 | 2.96 | 2.62 |
| 16:00 | 4276 | Namungo vs Azam | 3.21 | 2.64 | 2.44 |
| 16:00 | 5144 | Rhodos FC vs AEK Athens B | 2.39 | 2.80 | 3.09 |
| 16:00 | 5215 | APS Zakynthos vs O F Ierapetras | 2.01 | 3.22 | 3.42 |
| 16:20 | 4728 | Al Orubah vs Alshoulla | 2.60 | 2.84 | 2.75 |
| 16:30 | 5232 | Jomo Cosmos vs Polokwane City | 4.44 | 3.24 | 1.77 |
| 16:30 | 5235 | PSS Sleman vs Psis Semarang | 3.03 | 2.84 | 2.39 |
| 16:30 | 5303 | Anagennisi Derynia FC vs Alki Oroklini | 5.20 | 3.40 | 1.75 |
| 17:00 | 2161 | Tiddim Road Athlectic Club vs Kenkre FC | 1.23 | 5.40 | 9.63 |
| 17:00 | 3199 | Palermo vs Fidelis Andria | 1.62 | 3.67 | 5.56 |
| 17:00 | 5850 | Pescara Youth vs Napoli Youth | 3.80 | 3.80 | 1.74 |
| 18:00 | 1427 | Senica vs FK Pohronie | 1.74 | 3.85 | 3.75 |
| 18:00 | 3399 | Tshakhuma vs Chippa Utd | 2.31 | 2.99 | 3.19 |
| 18:30 | 1229 | AL Sahel SC vs AL Nahdha | 2.02 | 3.03 | 3.65 |
| 18:30 | 1666 | Sekhukhune United vs Maritzburg Utd | 2.06 | 2.84 | 4.11 |
| 18:30 | 2904 | Borussia Dortmund U19 vs Atletico Madrid Youth | 2.17 | 3.84 | 2.64 |
| 18:30 | 5949 | El Ittihad Alexandria vs Ismaily SC | 2.57 | 2.97 | 2.87 |
| 18:50 | 1620 | Najran SC vs AL Adalh | 2.70 | 2.79 | 2.70 |
| 20:00 | 2526 | Wolfsberger AC vs RB Salzburg | 5.21 | 4.25 | 1.49 |
| 20:00 | 5621 | Jihlava vs Usti Nad Labem | 2.19 | 3.23 | 2.99 |
| 20:30 | 1839 | Mainz vs Borussia Dortmund | 3.93 | 3.83 | 1.82 |
| 20:30 | 2547 | Perugia vs Spal | 1.91 | 3.30 | 3.94 |
| 20:30 | 2800 | Cremonese vs Pordenone | 1.39 | 4.32 | 7.65 |
| 20:30 | 4133 | Orlando Pirates vs SuperSport Utd | 1.73 | 3.00 | 5.90 |
| 20:30 | 5086 | Ascoli vs Pisa | 2.85 | 3.04 | 2.50 |
| 20:45 | 3036 | KFC Oosterzonen vs KVC Westerlo | 4.20 | 3.71 | 1.73 |
| 21:00 | 2181 | Viktoria Berlin vs Zwickau | 2.74 | 3.33 | 2.41 |
| 21:00 | 3850 | Enppi Club vs Ceramica Cleopatra | 2.22 | 3.11 | 3.30 |
| 22:30 | 4412 | Brighton vs Tottenham | 3.16 | 3.26 | 2.29 |
| 22:45 | 2485 | Peterborough vs Swansea | 3.44 | 3.39 | 2.02 |
| 22:45 | 2496 | Coventry vs Hull City | 1.60 | 3.74 | 5.31 |
| 22:45 | 3748 | Nottingham vs QPR | 1.92 | 3.43 | 3.73 |
| 22:45 | 3899 | Albion Rovers vs Kelty Hearts FC | 6.19 | 4.35 | 1.41 |
| 22:45 | 4486 | Millwall vs Huddersfield | 2.40 | 2.99 | 3.04 |
| 22:45 | 5405 | Cardiff vs Stoke City | 2.42 | 3.15 | 2.86 |
| 22:45 | 5407 | Luton Town vs Preston | 2.22 | 3.08 | 3.28 |
| 22:45 | 5819 | Blackpool vs Sheffield Utd | 3.34 | 3.19 | 2.14 |
| 23:00 | 4083 | Lille vs Chelsea | 4.10 | 3.60 | 1.86 |
| 23:00 | 5826 | Juventus vs Villarreal | 2.02 | 3.33 | 3.77 |
| 23:15 | 1670 | Arsenal vs Liverpool | 3.77 | 3.82 | 1.88 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# WAWILI WAJISHINDIA MAMILIONI BET BONANZA

**Na Mwandishi Wetu**

JUMLA ya washindi wawili kutoka Vodacom na Airtel, wameibuka washindi wa vitita vya shilingi milioni moja kila mmoja katika droo ya kwanza ya wiki ya Bet Bonanza ya Sportpesa iliyochezeshwa jana.

**Droo hiyo ni sehemu ya Promosheni ya Bet Bonanza ya Sportpesa, na pia ni mwendelezo wa zawadi ambazo zinatolewa katika kipindi hiki ambapo kuna ligi mbalimbali zinazochezwa kwa ushirikiano na Kampuni za simu za Vodacom, Airtel na Halotel.**

Akizungumza baada ya droo hiyo iliyochezeshwa Makao Makuu ya Sportpesa Oysterbay jijini Dar es Salaam jana, Meneja Uhusiano wa Sportpesa, Sabrina Msuya alianza kwa kuwapongeza washindi hao kwa kuibuka washindi wa wiki ya kwanza ya promosheni hiyo.

"Kwa hakika Watanzania hawa wawili wamejishindia vitita hivi vya shilingi milioni moja, wateja wenzao ambao wanatumia huduma za makampuni haya kuendelea kucheza mara nyingi kadri iwezekanavyo ili na wao washinde zawadi hizi," alisema Sabrina.

Aliwataja washindi hao kuwa ni Seif Ramadhani kutoka Shinyanga na Nyange kutoka Tabata.

"Nawasisitiza Watanzania hasa wateja wa Vodacom, Airtel na Halotel, kutumia fursa ya promosheni hii ya Bet Bonanza kwani kuna zawadi ya shilingi 20,000 kila siku, zawadi ya shilingi milioni moja kwa washindi watatu kama hili kila wiki na zawadi kubwa kabisa ya Sh. 15,888,000 siku ya kufunga promosheni,"alisema Sabrina.

Ikumbukwe promosheni hii ilizinduliwa rasmi wiki iliyopita inajumuisha zawadi za shilingi 20,000 kila siku, zawadi za milioni moja moja kwa washindi watatu kila wiki, na zawadi ya Sh.15,888,000 siku ya kufunga kampeni.

Ili kujisajili na kucheza na ***Sportpesa*** Piga ****150*87#*** au tembelea ***www.sportesa.co.tz*** au download APP ya ***SportPesa***. Kwa msaada zaidi piga huduma kwa wateja ***0764115588*** na ***0685115588***




Meneja Uhusiano na Mawasiliano SportPesa Tanzania, Sabrina Msuya, akitangaza washindi wa wiki ya kwanza wa Promosheni ya Bet Bonanza ikiwa ni mwendelezo wa promosheni hiyo ambapo kila siku hutangaza washindi wa Sh. 20,000 na mwisho wa promosheni atatangazwa mshindi wa Sh. 15,888,000. **MPIGAPICHA WETU**

# *Kibu apania kupambana kumshawishi Pablo*

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Simba, Kibu Denis amesema atahakikisha anajituma na kufanya vizuri kila akipewa nafasi aweze kuendelea kulishawishi benchi la ufundi kumchezesha hasa katika michuano ya kimataifa.

Kibu alikuwa miongoni mwa wachezaji walioanza dhidi ya RS Berkane mwishoni mwa wiki, ambapo kwake hiyo ni mechi yake ya kwanza kucheza katika michuano hiyo ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Nyota huyo usajili wake wa CAF ulichelewa kutokana na matatizo yake ya uraia, hali iliyosababisha kutoitumikia klabu yake hiyo kwenye mechi za awali, lakini baada ya kukamilika alikumbwa na majeraha hivyo kukosa mechi tatu za hatua ya makundi kabla ya Jumapili kuichezea Simba kwa mara ya kwanza wakati ikiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya RS Berkane katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kibu alisema, anafuraha kucheza mechi yake ya kwanza ya kimataifa kwa ngazi ya klabu katika mchezo wa mwishoni mwa wiki wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya RS Berkane. Alisema kila mchezaji furaha yake ni kucheza mechi kubwa za Afrika kama ilivyokuwa kwake na anaamini ataendelea kujituma zaidi ili kumshawishi Kocha Mkuu, Pablo Franco kumwamini na kumpa nafasi katika michezo ijayo.

"Ni furaha kubwa kwangu kucheza mechi yangu ya kwanza ya kimataifa ya mashindano ya ngazi ya klabu, kila mchezaji anatamani kupata nafasi ya kucheza michuano hii, naamini mwalimu ataendelea kunipa nafasi," alisema Kibu.

Alisema anaamini Simba itafanya vizuri katika michezo iliyobaki ya kimataifa kwa sababu wamedhamiria kupambana kila mechi kwa ajili ya kutafuta pointi ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kufuzu hatua ya robo fainali.

Simba inaongoza Kundi D ikiwa na pointi saba, pointi moja mbele ya Asec Mimosas na RS Berkane huku Us Gendarmarie ya Niger wakiburuza mkia kwa alama zao nne.

Michezo

Jumatano Machi 16, 2022

Nipashe



Tepsi aitwa Stars, Nyoni, Msuva waachwa
UKURASA 20

MTAJUA HAMJUI!...



Pape Sakho (mbele), akishangilia kwa staili ya aina yake akiwa amekaa chini sambamba na Shomari Kapombe (kulia) na Henoc Ingonga, baada ya winga huyo raia wa Senegal kuifungia timu yake bao pekee wakati ikishinda 1-0 dhidi ya RS Berkane ya Morocco kwenye mechi ya Kundi D ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa mwishoni mwa wiki. **PICHA: SIMBA**

## Simba na kampeni ya kufuzu CAF ugenini

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imetangaza kampeni kabambe ya kutaka kufuzu robo fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika ikiwa kwenye ardhi ya ugenini nchini Benin itakapocheza dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast, Jumapili ijayo.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally amesema kwa kutambua umuhimu wa mechi hiyo, kikosi cha timu hiyo baada ya mapumziko mafupi iilipomaliza mechi ya Jumapili iliyopita dhidi ya RS Berkane ya Morocco, imeanza mazoezi jana (Jumanne) kujiwinda na mchezo huo ambao huenda ukatoa taswira halisi ya wawakilishi hao wa Tanzania kwenye michuano hiyo.

"Hatuna mchezo wa Ligi Kuu kwa muda wa wiki tatu, baada ya mechi dhidi ya RS Berkane tuliwapa mapumziko wachezaji wetu, waende wakafurahi na familia zao, kusalimia, waende wakapate raha, wakashangilie ushindi nyumbani kwao, yameisha na sasa wanarejea tena kujiandaa na mechi hiyo ambayo tumeipa umuhimu mkubwa sana kuliko mechi zote.

"Kampeni yetu sasa ni kwamba tumejiandaa kwenda kuifunga Asec Mimosas huko huko ugenini na kama tukishinda moja kwa moja tunaingia robo fainali, hii ina maana tunataka kufuzu ugenini, halafu mechi ya mwisho dhidi ya US Gendamarie itakuwa ni ya kusaka pointi tatu ili tufuzu tukiwa na pointi nyingi zaidi, pia itakuwa ni mechi burudani zaidi na ya kupongezana kama tukifanikiwa kufuzu ugenini," alisema Ahmed.

Meneja Habari huyo na Mawasiliano amewashukuru wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kwa sapoti kubwa waliotoa kwenye mechi ya Jumapili iliyopita, akisema kuwa ushindi na pointi tatu zilizopatikana pamoja na wachezaji kupambana, lakini umechangiwa zaidi na mashabiki waliojitokeza kwa wingi uwanjani.

"Zile kelele, ushangiliaji, na hamasa ndizo zilizowatoa Waarabu mchezoni na kuwafanya wapate shida, wakafanya vurugu, wakataka kususa na kutoka uwanjani," alisema.

# Mayele amtuliza mzuka Nabi

## ●●● Aahidi kutetema hadi mbio za Kiatu zieleweke Ligi Kuu, atuma salamu KMC, lakini...

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amekuja juu akiwaweka kitimoto wachezaji wake na kuwataka kutofanya makosa katika kila mchezo hususan Jumamosi dhidi ya KMC FC, lakini mshambuliaji kinara wa timu hiyo, Fiston Mayele, ni kama amemtuliza mzuka baada ya kuahidi kuendeleza kasi yake ya 'kutetema' hadi kieleweke.

**Yanga ambayo ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na alama 45, nane zaidi ya watani zao, Simba waliopo nafasi ya pili, itashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumamosi kuvaana na KMC FC katika mwendelezo wa ligi hiyo.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema kila mmoja anajua uwezo wa KMC FC ambayo ni miongoni mwa timu bora kwenye Ligi Kuu na wanatarajia kuwa na mchezo mgumu.

Alisema ushindani na ugumu wa mchezo huo hautampa presha hasa kutokana na ukweli kuwa sehemu kubwa ya kikosi chao kina wachezaji wazoefu, lakini hilo haliwezi kuwa sababu ya kubweteka.

"Lakini licha ya ushindani tunaotarajia kukutana nao, ni lazima tuhakikishe tunashinda mchezo huu, ni lazima mawazo yetu yawe juu ya pointi tatu na si matokeo ya aina nyingine na wachezaji wangu wanajua hilo," alisema Nabi.

Alisema ligi imekuwa na ushindani mkubwa kwa sababu kila mmoja anahitaji kupata matokeo mazuri hali ambayo wanapaswa kuwa makini kuhakikisha wanaendelea kupata pointi katika mchezo huo.

Nabi alisema wachezaji wanatakiwa kutambua umuhimu wa kila mechi na kusahau matokeo ya mechi zilizopita na sasa kuanza moja kwa kutafuta alama tatu dhidi ya KMC ambao nao wanatafuta pointi ili kujiweka katika nafasi nzuri katika msimamo.

Wakati Nabi akizungumza hayo, mshambuliaji wa timu hiyo, Mayele ameahidi kuendelea kutetema (kufunga) katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC dhidi KMC pamoja na michezo mingine iliyopo mbele yao.

Mayele aliliambia gazeti hili kuwa lengo lake ni kuisaidia timu na kisha kutwaa Kiatu cha Dhahabu kwa kuibuka mfungaji bora wa Ligi Kuu.

"Lengo langu ni kuchukua Kiatu cha Mfungaji Bora msimu huu, licha ya kwamba kuna ushindani mkubwa, nikishirikiana na wachezaji wenzangu inawezekana," alisema Mayele.

Naye Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, alisema timu yao inaendelea kujinoa kuelekea mchezo huo wa Jumamosi ambao watakuwa wenyeji dhidi ya KMC iliyopo nafasi ya saba ikiwa na alama 22 kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Wachezaji wanaendelea na mazoezi kujiandaa kukutana na KMC, kocha amesema kila mchezo kwetu ni fainali kwa kuwa mikakati yetu ni kutwaa ubingwa msimu huu, " alisema Bumbuli.

Bumbuli alisema wachezaji walianza mazoezi Jumatatu ya kurejea majumbani, lakini wakaingia kambini rasmi jana, Jumanne kwa ajili ya mechi hiyo.

Kuhusu hali za majeruhi alisema kwa sasa wapo wanne tu, huku wawili hali zao zikiendelea kuwa vizuri na huenda wakaonekana Jumamosi kwenye mechi hiyo.

"Wachezaji ambao ni majeruhi ni Khalid Aucho na Saido Ntibazonkiza ambao hawakuonekana kwenye mechi iliyopita, lakini hali zao kwa sasa ni nzuri na wanaweza kuonekana kuanzia mechi zinajazo, wapo pia majeruhi wa muda refu kidogo ambao ni Yacouba Songne na Jesus Moloko," alisema Bumbuli.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >